

KITABU CHA UZIMA

CHA MWANA-KONDOO

 Habari ya asubuhi, marafiki. Lilikuwa kidogo ni jambo la kushangaza kwangu kuwa hapa leo. Sikuwa nikitarajia kuwa hapa. Nilikuwa niwe huko Kentucky. Ndipo rafiki yangu mpendwa sana akawa mgonjwa sana, Ndugu yetu Lyle McSpaddin. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . hali ya kufa hospitalini. Bibi Ferguson ambaye alizoea kuja hapa, mwanawe akifa, pia, hospitalini. Na kwa hivyo sikuenda, nami nikabaki tu kwa ajili yao.

² Na kisha Bw. Matheny wa kanisa la Kipentekoste huko New Albany, kwenye Barabara ya Silver, nyuma tu ya . . . Ni kati . . . Iko kwenye Oak na Silver, nadhani. Naye . . . Nilipaswa kumzungumzia usiku wa leo, nami nikamwambia . . . Nikaubatilisha, Jumatano iliyopita, na kumwambia ya kwamba ningengoja hadi nirudi kutoka Indianapolis. Ndipo basi nilipokimbia tu hospitalini jana, kumwona Ndugu Lyle, mbona, nilikutana naye. Naye akasema, “Vema, naona hukuenda.”

Nami nikasema, “La.”

Akasema, “Vema, njoo, ukahubiri, kwa vyovyote vile.”

³ Kwa hiyo, nadhani, Bwana akipenda, nitakuwa chini kule usiku wa leo, kuzungumza kwa niaba ya Ndugu Matheny. Na, naam, nilimwambia, ya kwamba tuliposhuka kwenda kule, ningemfanyia ibada ya uponyaji. Na kwa kawaida napenda kufunga siku tatu hivi kabla ya ibada ya uponyaji. Kwa hiyo nilimwambia nitazungumza, na kukiweko na mtu yeyote kule, tungewaombea, kwa vyovyote vile, m—mstari tu wa kawaida wa maombi.

⁴ Sasa, tuna juma moja zaidi, juma moja kutoka Jumatatu ijayo, sasa hadi ibada zitakapoanza kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis. Nasi tunatumaini ya kwamba Bwana atatubariki kule juu, katika mkutano mkubwa sana. Kama mtoto, mwenye matarajio ya Krismasi, ninangojea ibada hiyo. Mimi . . .

⁵ Ninyi, jambo fulani tu kuhusu kumtumikia Bwana, tunachoka sana wakati mwingine, mpaka inaonekana kana kwamba hatuwezi kwenda mbali zaidi. Na kisha unapopumzika, siku moja au mbili tu, kuna kitu kinakugusa na—na lazima uende tena. Kwa hiyo, leo hii, tuko hapa kwa kusudi moja, yaani, kumtumikia Bwana.

⁶ Na kabla tu hatujaomba na kulisoma Neno, ninataka kuomba msamaha hadharani kwa Ndugu Neville. Mimi... Jana, nilikaa nyumbani kutoka kule chini Kentucky, jana, kimakusudi, kuhubiri badala yake redioni. Jumamosi ijayo, na Mungu akipenda, pia Ndugu Neville akipenda, ninataka kuzungumza kwenye matangazo ya asubuhi Jumamosi ijayo, kwa niaba ya Ndugu Neville.

⁷ Na kwa hiyo, alikuwa mwenye neema sana kunisamehe, kwa urahisi. Alisema... Nadhani nilijinufaisha kwake, naye ni mmoja wa jamaa hao ambao wanaweza... Ninaweza kurudisha pongezi, na, "Namtarajia mtu." Na kilichonifadhaisha kilikuwa ni asubuhi hiyo na mapema waliponiita kwa Ndugu Lyle na wengineo, huko New Albany. Nami... Ilikuwa ni kama dakika kumi ifike saa tatu, nami nikasema, "Loo, nilipaswa kuwa kwenye matangazo hayo katika dakika kumi." Na hapa, mimi huko Jeffersonville, yeye kule chini akiningojea. Kwa hiyo mimi...

⁸ Ndugu Wood alimpigia simu jana, nami nikafikiri ningemwacha Ndugu Wood aniombee msamaha, kwanza, mwajua. Kwa hiyo akaniadhibu tu kunifanya nizungumze asubuhi ya leo, nishuke huku. Kwa hivyo sisi hapa. Na hivyo yeye... tunaninii...

⁹ Tunaamini ya kwamba—ya kwamba Mungu ata—atakuwa katika ibada zetu. Sina kitu nilichokusudia; hata sijui nianzite wapi katika Maandiko; nilichukua tu Biblia yangu muda mfupi uliopita, nikaja mbio. Ilinibidi kuchukua Biblia yangu ya Collins, kwa sababu ina maandishi makubwa zaidi.

¹⁰ Jamani! Nimepita arobaini, mnajua. Kwa hiyo, unapofikia umri wa miaka arobaini, chochote kilicho karibu nawe, hukioni kama ulivyokuwa ukiona, unajua. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa ni kweli? Naam. Naam, bwana.

¹¹ Hapa si muda mrefu uliopita, niliwazia, "Aisee, nina shida fulani, siwezi kuvaa miwani ya kijani au miwani ya kahawia." Sikuweza kamwe; inanichefua tumboni mwangu. Kwa hiyo nikasema, "Kuna kasoro." Nilimpigia simu Dk. Adair, nami nikasema, "Dak, rangi gani... Unaweza kuyachunguza macho yangu, uniambie ninapaswa kuvaa miwani ya rangi gani?"

¹² Akasema, "Mimi, hebu nikwambie." Akasema, "Nitakwambia. Nitakutuma tu kule Louisville, kwa mtaalamu fulani huko, kuhusu hilo."

¹³ "Vema," nikasema, "Sitaki uchunguzi wowote wa macho." Nikasema, "Nina macho mazuri. Ninaweza kusimama na kuona unywele ukiwa sakafuni."

¹⁴ Akasema, "Lakini, afadhali akufanyie uchunguzi, kwa vyovyote vile, naye atakwambia ni rangi gani unayopaswa kuwa nayo."

¹⁵ Kwa hiyo, nikaenda huko. Na, nikapata kujua, yeye alikuwa ni ndugu Mkristo, alitaka kurudi Afrika pamoja nami na kufanya upasuaji. Kasema, “Sasa, hao wenyeji ni wa ajabu sana, unaona.” Kasema, “Hawataruhusu kisu kiwakate.” Lakini wanakupenda. “Nami ninataka kutoa huduma ya bure kwa miezi sita, ya kuondoa mtoto wa jicho na vitu kama hivyo, kwa hao wenyeji.” Naye akasema, “Utakapoenda huko,” kasema, “Ningependa kutoa miezi sita ya maisha yangu kwa utumishi wa Bwana.”

Nilisema, “Dak, unaamini katika uponyaji wa Kiungu?” Akasema, “Kila neno lake.”

¹⁶ Naye akanipa ushuhuda, kuhusu wakati mmoja ambapo... Alikuwa mtaalamu wa koo na macho. Akasema walimpigia simu. Mtoto mchanga alikuwa amemeza moja ya vijifilimbi hivyo, nacho kikakwamia kooni mwake. Kasema, “Nikaenda huko, naye huyo mtoto alikuwa tu anaondoka. Wakamkimbiza hospitalini. Hakuna kitu ungaliweza kufanya.” Kasema, “Sikujua la kufanya. Kwa hiyo,” kasema, “Nilinini tu, nikatoka nje ya chumba, nami nikasema, ‘Mpendwa Baba wa Mbinguni, nisaide kujua kwa njia fulani nini cha kumfanyia maskini mtoto huyo. Yuafa. Wala siwezi kupata chochote karibu naye, kumshtua, wala sijui la kufanya.’” Kisha akasema, “Huyo mtoto mchanga akafanya, ‘Uh!’ Na hicho kijifilimbi kikaruka mpaka sakafuni. Kwa hiyo,” akasema, “ningewezaje kujizua kuamini?” Maombi hubadilisha mambo. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, akaniambia. Tukaketi pale na kuongea kidogo.

¹⁷ Naye alikuwa na kile chumba kidogo chenye giza, akafanya kitu hicho kidogo kuja, nami nikaona ile taa ndogo nyekundu. Akasema, “Je, unaweza kusoma hilo?”

¹⁸ Nakaona kilisema ishirini kwa ishirini. Nikasema, “Naam, bwana.” Ningeweza kuisoma, kwa vyovyote vile, ishirini kwa ishirini. Kisha akaweka kumi na tano kwa kumi na tano, ningeweza kuisoma. Na kumi kwa kumi, ningeweza kuisoma.

¹⁹ Kasema, “Vema, macho yako hayana shida sana.” Kisha akaweka darubini ndogo hapa nje, pamoja na... Kasema, “Nisomee hiyo.” Nami nikaiona, ningeweza kuisoma vizuri. Akaendelea kukaribia zaidi, zaidi. Usomaji wangu ukaanza kupunguka. Alipofikia karibu *hivi*, nikaacha. Akasema, “Nitakwambia, kabla sijakuuliza. Umevipita arobaini.”

Nikasema, “Naam. Hiyo ni kweli.” Nikasema, “Nina arobaini na tano.”

²⁰ Naye akasema—akasema, “Vema, mtu anapopita arobaini...” Kasema, “Sioni jinsi ulivyoliepuka kwa muda mrefu hivi.” Kasema, “Kama vile tu nywele zako zinavyoingia mvi, ngozi yako ikakunjamana, nywele zikatokea masikioni mwako, na kadhalika.” Bw. Egan anaweza kukwambia hilo, kama kinyozi. “Basi unapopita umri wa miaka

arobaini,” kasema, “mboni za macho yako zinakuwa bapa na hazitapanuka.” Kasema, “Sasa nitakwambia jinsi ya kufanya hivyo. Vema, sasa, finya macho yako sana, na usome hili.”

²¹ Vema, ndugu, ningeweza kulisoma, kama lilikuwa karibu *hivyo* nami, nikiyafinya macho yangu. Nikaiweka mikono yangu namna *hiyo*, na kufanya kitu kama darubini ndogo, ungeweza kuisoma. Macho yako hayana shida. Ni maumbile tu, umri wa miaka arobaini, watu hawana budi kuvaa miwani ya kusoma.

²² Na kwa hiyo alitaka kunitengenezea moja. Na, vema, alinitengenezea. Lakini kamwe si—sikupenda vitu hivyo, mnaona. Wala si—sikuzote siwazii, nami husoma wakati mwingine. Na, lakini, nilijitwalia tu Biblia ya Collins, ambayo ni ma—maandishi makubwa kidogo. Nami nikawazia, “Vema, siwezi kuzoea kuivaa, mnaona.” Nawe hu—huangalii... Kama ningeangalia kando, nje namna *hiyo*, huwezi kuona chochote. Lakini ukiangalia chini kwa karibu, basi inakuletea.

²³ Kasema, “Sasa, unaanza kusoma *hivi*,” kasema, “muda si muda mwajua, unaendelea kurudisha mkono wako nyuma. Kwa umbali *huo*, mkono wako si mrefu kutosha, ili ukifikie.” Kwa hiyo, hivyo—hivyo ndivyo ilivyo.

Na kwa hivyo, sasa Bwa—Bwana awabariki.

²⁴ Sasa nataka kuwauliza jambo fulani, asubuhi ya leo, kabla hatujaanza somo la shule ya Jumapili. Thamani ni—ni nini? Nimekuwa nikiliwazia. Kama ningekuwa na koo la kutosha asubuhi ya leo, ningehubiri juu ya somo hilo. Lakini, koo langu, mbaya, nami nina mkutano huu unaokuja hapa, New Albany, usiku wa leo. Na halafu, pia, nina ninii... Miamsho inaanza. Ninataka tu kufundisha kwa muda, asubuhi ya leo, kutoka kwenye Maandiko fulani. Lakini, thamani ni nini?

²⁵ Mama yangu, sidhani yuko hapa. Simwoni popote. Yuko? Naam, mama, unakuwa mdogo. Kwa hiyo, nilimuuliza jana. Nilimuuliza hili somo, maana nimekuwa nikilichunguza. Ukipata jambo niani mwako, unaanza tu kusoma? Ndugu Weber, ulifanya hivyo mara nyingi, ndipo unaanza tu kusoma.

²⁶ Thamani ni nini? Nami nikaanza kuwazia. Nikasema, “Unajua, kama ningalikuwa na dola milioni mia moja zimewekwa hapa katika lundo, nami nilikuwa na kitufe kidogo hapa. Kama nikibonyeza kitufe hiki, ninapoteza dola zangu milioni mia moja, lakini ninapata kuzungumza na maskini baba yangu ambaye ametuacha, kama saa moja, akiwa mwanadamu aliye hai tena. Ningefanya nini?” Bila kusita, ningebonyeza hicho kitufe. Ningetoa dola milioni mia moja, asubuhi ya leo, kumketisha baba yangu kwenye kiti hiki, wakati nikilifundisha somo hili. Kwa hivyo pesa ina thamani gani? Nafsi ina thamani sana vipi kuliko pesa? Mnaona?

²⁷ Sasa, mama, unakumbuka nilipokuwa na ile Ford ndogo ya kale Muundo T, maskini muundo wa '26? Jinsi ningepiga msasa

kitu hicho! Nilikuwa tu mtoto, yapata umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba. Nilikuwa mwenye dhambi wakati huo. Na wakati mwingine... Nilikuwa nikifanya kazi na Bw. Genther kule nyuma. Na ningeninii... Baada ya Jumapili alasiri... Jumapili asubuhi, ningeshuka kule na kung'arisha sehemu zote na kila kitu, kwa kompresa ya hewa, na kuisafisha. Jumapili alasiri, ningeing'arisha maskini hiyo Ford kuukuu, mpaka ilionekana kana kwamba ingetoka rangi. Vipi kama ningejaribu, asubuhi ya leo, kutafuta kipande kimoja cha hiyo Ford? Vipi kama ningejaribu kutafuta moja ya vipande hivyo, kutoka kwenye kompresa hiyo ya hewa? Wakati ningeikuwa nikiwaleta watu, nilikuwa nikiisafisha Ford yangu. Nashangaa thamani iko wapi.

²⁸ Nilifanya kazi Jumapili asubuhi kule juu, kadiri walivyoniruhusu. Niliithamini, kwa sababu nilikuwa na deni. Nami... Lakini ilinifikisha wa—wapi? Je, ilileta nini?

²⁹ Ndugu Ledford, vipi kama mtu fulani akija kwangu mimi na wewe, na Ndugu Neville, asubuhi ya leo, sisi sote hapa, sisi watatu, hasa, na kusema, “Wahudumu, nitawapa kila mmoja wenu dola milioni moja.” Mtu aliyekuwa na uwezo... angeweza kulifanya.

³⁰ Nami nikasema, “Sasa, Ndugu Ledford, Ndugu Neville, niwaambie jambo tufanye. Twendeni tukawatafute maskini wote tuwezao. Na tufanye kila makazi kuwa na furaha, kwa kuwapa watoto nguo, na kulipia rehani, au kununua mahali hapa padogo. Hatungezikosa. Dola milioni moja kwa kila moja, mbona, riba yake, tuwashughulikie wengi tuwezao nazo; tuziweke katika uwekezaji mzuri au chochote kile. Ndipo tungefanya nini? Hilo lingekuwa sawa, kwamba, tusiruhusu mtu yeyote ajue lolote kulihusu. Mioyo yetu ingejisikia kuridhika.

³¹ Lakini, sasa, katika miaka mia moja kutoka leo, ndugu, ingehitaji muujiza wa Mungu, kama bado tunaishi miaka mia moja kuanzia leo, mnajua hilo. Sasa, tungekuwa katika Umilele. Je, hizo dola milioni moja zingefaa nini, ama kuwalisha maskini, na mambo tuliyofanya? Mnaona? Hazitafaa kitu. Kama ningalikuwa na bilioni, asubuhi ya leo, ingetufaidi nini baada ya sisi kuondoka?

³² Lakini hebu niwaambie jambo fulani. Hatuna pesa hizo. Wewe ni maskini; sisi sote hapa. Hiyo ni kweli. Tunaishi kwa misaada ya watu, tukiwa wahudumu. Lakini ndugu, huko Afrika, mvulana mmoja mweusi wa kimo *hiki*, ama kahaba mtaani huko Louisville, nafsi moja iliyookolewa; katika Umilele, wakati nyota hiyo inapong'aa kule, jina letu litafunganishwa ndani yake. Hiyo hapo thamani yako. Sio kiasi ulicho nacho, kiasi gani unachotamani. Ni yale unayoweza kufanya kuokoa nafsi kwa ajili ya Kristo Yesu. Pesa zetu zitatoweka.

³³ Niliipiga msasa maskini hiyo Ford kuukuu. Na asubuhi ya leo, Kadilaki ambayo wao walinipa imewekwa kule kwenye gereji. Lakini moja ya siku hizi, hiyo Kadilaki itakuwa kama ile Ford ilivyo, haitakuwapo tena. Lakini Mungu angali atakuwa yeye yule. Lakini, nikiifanya nafsi moja kuokoka kwa ajili ya Kristo, ndugu, maadamu kuna Umilele, utukufu wa Mungu utakaa juu ya nafsi hiyo.

³⁴ Kwa hivyo, thamani ni nini, kwa vyovyote vile? Je, inafaidi nini, wakati mapambano yapo kwenye koo lako, huku daktari anaona mdundo ukipitia mkononi mwako? Pesa zote na umaarufu wote una faida gani? Watu wa kukupigapiga mgongoni, au unakuwa mtu mkubwa, hiyo ina faida gani kwako? Si hata kidogo. Inatoweka, na kubaki hapa duniani.

³⁵ Lakini, nafsi moja iliyoookolewa, utaona jina lako limefungwa ndani yake, maadamu nyota ya asubuhi itametameta angani. Kwa hiyo, na tuwaokoe watu, ndugu. Kila mmoja, ninyi wake wa nyumbani, si lazima uwe mhubiri; wewe fanya jambo fulani kwa utukufu wa Mungu. Kumbuka, mambo ya Milele ndiyo yadumuyo milele, na, hiyo ni kusema, kuwaokoa watu. Hebu hilo liwe jambo la kwanza, kati ya kazi yako yote na mawazo yako yote na malengo yako yote.

³⁶ Jana, nikisimama karibu, nikishikilia mkono wa mama mmoja, nimemshika mkono, huku kidevu chake kikitetemeka.

³⁷ Naye mvulana wake amelala pale, akifa, akasema, "Billy, ni—nimetamani na kutamani sana urudi maskanini."

³⁸ Nikasema, "Dada Fergerson, ni—ningependa kufanya hivyo." Akasema... Nikasema, "Vema, angalia, dada. Ambapo ningeweza kupata labda watu hamsini walioookolewa, kwa mwaka, maskanini, hayo yangukuwa ni mazao mazuri kwa mwaka mzima. Ninaweza kupata laki moja waliookoka katika nchi nyingine. Unaona?"

³⁹ Nitakapoingia Utukufuni, sitaki... Mungu angeweza kuniokoa. Tayari ameniokoa. Hilo limetosha. Lakini jambo ni kwamba, nitakapofika kule, nataka kutazama huku na huku na kuona nyota zikiangaza. Amina. Na—nataka kuona kitu kinachofanya kitu.

⁴⁰ Kama mimi—kama nilikuwa nimekufa, na nilikuwa mtu mashuhuri, rais kama Lincoln, ama kitu kama hicho, wangejenga, ukumbusho mkubwa; lakini siku moja haungekuwako. Lakini nafsi moja iliyoookolewa, Utukufuni, jina lako litafunganishwa nayo, maadamu kuna Umilele unaobingirika humo.

Vema, na tuombe sasa.

⁴¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja Kwako kwa unyenyekevu sana, asubuhi ya leo. Mungu, nina furaha kwamba niliamka, yapata miaka ishirini na mitano iliyopita, kwa ukweli kwamba—

kwamba furaha haitegemei mambo ya ulimwengu huu. Inategemea mambo ya Milele, ambayo hutufanya tuwe na furaha nafsini mwetu.

⁴² Na jinsi nilivyo na shukrani, asubuhi ya leo, na ninakushukuru Wewe, kwa wokovu Wako na neema Yako, ambazo zimeniruhusu, Bwana, kuona karibu watu milioni moja wakipiga magoti madhabahuni. Ee Mungu, siku moja tukufu, nitakapovuka ng'ambo, ninatumaini kuwaona wote wakiangaza kule, kama nyota. Ndugu zangu hapa, dada zangu, asubuhi ya leo, kila mmoja anajisikia vivyo hivyo. Walikuwa na sehemu katika hilo, Bwana, kwa maombi na dua zao, na kumshikilia Mungu; kuomba, kuzungumza na wengine, na kuyasifu mambo ya Mungu.

⁴³ Nasi tunatumaini, leo, Mungu, kama kuna yeyote humu ndani ambaye hayuko pale tu anapopaswa kuwa, au bado hajamkubali Kristo kama walivyopaswa kufanya, jalia hii iwe ile siku ambayo uamuzi wao wa Milele, usio na kikomo utakapofanywa, kukutumikia Wewe. Tujalie, Baba.

⁴⁴ Jalia kila Mkristo, humu ndani, jalia moyo wao uwake ndani yao, waende nje mahali fulani, vichochoroni na njia kuu, wakawalete watu waliopotea, haijalishi ni nyenyekevu jinsi gani, wanaweza kuleta nafsi moja ambayo ingeleta milioni moja nyuma yake. Hatujui tunachofanya. Wakati mwingine maskini hawa akina mama hushangaa, Bwana, lakini hawajui wanalozungumzia, wanapozungumza na kijana, au mtu mzima, ama wowote wale kuhusu nafsi zao. Tujalie, Bwana.

⁴⁵ Sasa ingia katika Neno. Bwana, Wewe uko katika Neno. Na utupe imani ya kulifanya Neno liishi na kutenda, leo, maishani mwetu, katika nafsi zetu. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

⁴⁶ Sina hakika kama ilikuwa Dwight Moody. Ninaamini ndiye, yule fundi viatu wa Boston, ambaye siku moja... Maskini mwanamke mmoja, katika siku za mwanzoni za Kimethodisti, alitaka kumfanya Bwana jambo fulani. Kwa hivyo, alikuwa anafua nguo, naye akaweka akiba pesa zake, akapata dola moja na nusu, ninaamini, apate kumleta mhubiri mmoja mzee kumhubiria. Naye alikuwa amekodi banda la farasi, kwa robo ama chochote kile, usiku huo. Akalisafisha hilo banda, na kuweka chini be—benchi ndogo ya kufulia, kama madhabahu.

⁴⁷ Na kuwaonyesha tu jinsi ilivyo rahisi, kwenu wake wa nyumbani, sasa. Mnaona? Mnasema, "Loo, Ndugu Branham, laiti ningaliweza kuhubiri!" Sio lazima. Wewe ninii tu... Wewe ni ushuhuda. Wewe ni ushawishi; maisha yako.

⁴⁸ Naye akachukua vitini, akaenda nje pembeni, akiutangaza huo mkutano, na kuvisambaza. Kila wakati mtu anapokishika, wangekitupa chini. "Mtakatifu anayejibingirisha! Mlokole!" Na kusonga mbele. Mnaona?

49 Maskini mvulana mmoja akaja, akiwa na suruali chakavu. Vining'iniza suruali vya baba yake mabegani mwake; nywele zikining'inia usoni mwake. Kasema, "Mama, unasambaza nini?"

Kasema, "Kitini, mwanangu." Akamkabidhi, namna *hiyo*. Akakitazama, akasema, "Siwezi kusoma."

Kasema, "Vema, kinasema kutakuwako na mkutano usiku wa leo, hapa juu." "Loo," kasema, "kweli? Ungetaka nije?" Kasema, "Unataka? Lazima uje, mpenzi, ukiweza." "Sawa, nitafanya hivyo."

50 Usiku huo, baada ya juhudi zake zote, na ni dhaifu. Yule mzee mhudumu mwaminifu akaja, akaingia mimbarani na kuomba. Akaimba wimbo, yeye na huyo mama, naye ameketi huko nje kama kusanyiko lake.

51 Baada ya kitambo kidogo, huku akiyumbayumba mlangoni, akaja yule kijana mwenye sura chakavu, nywele zikining'inia usoni mwake. Unajua huyo alikuwa nani? Dwight Moody. Usiku huo, alipiga magoti madhabahuni; aliwaleta watu milioni moja kwa Mungu. Unaona? Hujui unachofanya.

Sema neno dogo kwa ajili ya Yesu
Shuhudia, imba, au uombe,
Na kama mkate juu ya maji
Utakurudia siku moja.

52 Hiyo ni kweli. Vema. Kumbuka tu, usikose, usikose; wavute watu! Chochote ufanyacho, wavute watu. Ni—nina furaha kuwaona watu wetu hapa, asubuhi ya leo, hakuna mmoja wao katika umaskini, nijuavyo mimi; wote wamevaa nguo nzuri, nanyi ni safi; watu wanaoonekana werevu. Ninamshukuru Mungu sana, kujua kwamba ndivyo mlivyo.

53 Nilikuja hapa, marafiki, wakati mmoja, wakati wa kuzorota kwa uchumi, wakati nilipohubiri huku nimevaa ovaroli. Nanyi mlitembea kwa maili kadhaa, hapa ndani, na kuvuka nchi, huku hamna chakula cha kutosha. Nami najua. Hiyo ni kweli. Nakumbuka hilo. Mungu ametubariki, nasi tunamshukuru, unaona.

54 Lakini asubuhi ya leo, mnaona, jinsi mnavyoonekana tofauti asubuhi ya leo, ninashukuru kwa hilo, lakini kamwe msiruhusu hilo liwazuie. Kumbuka ilikotoka, kutoka juu. Basi, okoa nafsi, Humo hiyo itadumu milele. Na labda sehemu kubwa yenu pengine ina akaunti ndogo ya benki mahali fulani. Nina furaha kwa ajili ya hilo, na Mungu na alibariki sana hilo. Lakini usiruhusu hilo likuzuie kuokoa nafsi. Hiyo ni kweli. Zitangulize nafsi.

55 Sasa nilikuwa nikiwazia labda... Nilimuuliza Ndugu Neville. Ama, huna somo fulani la shule ya Jumapili, kwa hiyo tutafundisha tu kutoka popote, na mahali fulani katika Biblia. Nami niliwazia kuhusu kufundisha, asubuhi ya leo, nilipokuwa

nikishuka, kabla sijaingia chumbani, kuhusu, kwenye Kitabu cha Ufunuo.

⁵⁶ Kisha nikakumbuka kwamba kipindi fulani cha redio kinaendeleza m—mfululizo juu ya Kitabu cha Ufunuo. Charles Fuller, nadhani, anafuatisha ki—kitabu. Naye Ndugu Fuller ni mtu wa mifano, yeye mwenyewe. Nami nilihofu kwamba kwa namna fulani tungekusanyika pamoja juu ya hilo, na tayari mmesikia baadhi yake.

⁵⁷ Kwa hiyo, basi, nilifikiri tungeenda kwenye Kitabu cha Waebrania. Ni kizuri...Ni wangapi wanapenda Kitabu cha Waebrania? Loo, ni kizuri...Hebu tufungue kwenye mlango wa 10 hivi. Nafikiri huo ni mlango wa kupendeza. Sijui kama nimewahi kufundisha juu yake, lakini labda nimefundisha, hapa, sehemu yake. Kwa kawaida tunachukua vifungu viwili ama vitatu, halafu hilo latosha, nasi tunaanza katika Biblia.

⁵⁸ Mnajua, wakati mwingine, ninapokuja likizoni, nina shauku sana ya kupata wakati mmoja zaidi, ambapo ningeweza kutulia humu maskanini, ama mahali fulani hapa, na kufanya tu mfululizo wa masomo, kama tulivyozoea kuichukua Biblia. Kama vile tu kwenye Kitabu fulani, tunakiendea tu, tunakichambua huku na huku kupitia kwenye Maandiko namna hii. Inaweka na kuimarisha Imani yetu. Hiyo ndiyo sababu ya masomo haya, ni kuiimarisha Imani yetu.

⁵⁹ Sasa, katika mlango wa 10 wa Waebrania. Sijui ni kwa nini, nikiketi tu pale ndani, niliufungua tu. Nasi tunataka kusoma kutoka hapa, kwa ajili ya somo dogo, na kulifundisha. Tukifika hapa chini, tujue tumeyapitia hapo awali, basi nitaninii... tutageuka tuliedee jambo lingine, au labda Bwana atatuongoza kwenye kitu kingine.

⁶⁰ Sasa msisahau ibada usiku wa leo humu maskanini. Ndugu atakuwa akizungumza nasi usiku wa leo. Na kama una marafiki wowote karibu na New Albany kule chini, kwa Ndugu Matheny, tutazungumza huko kwa muda kidogo usiku wa leo. Na kisha Jumatano usiku.

⁶¹ Na Ndugu Junior Jackson, nilimsikia akiitikia “amina” muda mfupi uliopita, lakini sijaweza kumwona. Naye yuko humu jengoni. Na yake ni Alhamisi usiku, na—na ninaamini ana Jumapili usiku. Uko wapi, Junior? Siwezi kuona ulipo. Loo, si ajabu; umeketi nyuma ya huyo jamaa mkubwa huko nyuma. Ninii yako...Kile...ibada yako Iju-...Jumapili usiku, pia, ndivyo, Junior? [Ndugu Jackson anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Alhamisi na Jumapili. Vema. Na ibada zake ni usiku wa leo, naye yuko kwenye Barabara ya Jimbo, huko New Albany. Jimbo na [“Monroe.”] Monroe.

⁶² Ndugu Genther, unaona ni muda mrefu tangu nisome mita, au kurekebisha huduma zozote. Nilisahau mitaa yote. Lakini

kuna... Bado ninampenda Bwana Yesu yeye yule aliyekuwa pamoja nasi wakati huo, aliponisaidia siku hizo.

⁶³ Nilikuwa nikimwambia ndugu mmoja, muda mfupi uliopita. Nilikuwa nikishuka pale nilipokuwa nasoma mita, na kubisha mlango. Ninasoma mita, kisha naitoa Biblia yangu na kusoma kidogo, kabla huyo mama hajafika mlangoni, kitu kama hicho. Kisha natafuta maskini jengo dogo la kale tupu. Bila shaka, huwezi kuyapata sasa, ambapo mtu fulani alikuwa amehama. Naingia mle, kisha naenda nyuma kwenye kibanda na kupiga magoti na kuomba. Huko kulikuwa ni kuandaa, hicho ndicho kilichoiimarisha pale, kumtegemea Yeye.

⁶⁴ Sasa, Kitabu cha Waebrania ndicho—ndicho kinachoitenganisha torati na neema. Ni wangapi wanajua ya kwamba tunaishi kwa neema, na wala si kwa sheria? Ninaamini mwandishi... Hakuna anayejua hasa. Lakini sana sana ni kama Paulo, mpaka ninapenda kuyaita maandishi ya Paulo. Naye alikuwa akizungumza na Waebrania.

⁶⁵ Sasa, Injili ilikuwa tayari imewaandea Mataifa, kwa maana Wayahudi walikuwa wameikataa. Nao walikuwa wamewaandea Mataifa pamoja na Injili. Na sasa Paulo alikuwa akiwaandikia Waebrania, kwa maana wengi wao walitaka kurudi chini ya sheria, kushika sheria, na bado wamwamini Kristo.

⁶⁶ Basi, unajua, hayo yangali yako siku hizi. Kuna watu siku hizi ambao wanajaribu kushika torati za Agano la Kale, na bado wawe Wakristo, wakati moja ni kinyume sana na hiyo nyingine. Kama ukitimiza sehemu moja ya torati, huna budi kutimiza yote. “Wewe ni mdeni,” inasema Biblia, “kutimiza torati yote,” kwa hiyo, kama unafanya sehemu yake. Halafu, basi, kama ukishika torati, kama vile dhabihu, na sabato, na wajibu, na ulaji, na kutawadha, na kadhalika, chini ya torati.

⁶⁷ Lakini hatuko chini ya torati sasa. Tuko chini ya neema. Naye Paulo anajaribu kuonyesha mahali ambapo torati ilikuwa ni kivuli. Sasa, hapo mwanzo, hapa tunaona jambo hilo.

Kwa maana torati, kwa kuwa ni kivuli cha mambo mema yatakayokuwako, wala si sura yenyewe ya vitu hivyo, haiwezi kamwe kwa dhabihu zile walizozitaa mwaka baada ya mwaka daima kumfanya ajaye kuwa mkamilifu.

⁶⁸ Loo, jamani! Je, hilo si lingefanya mahubiri papo hapo? Mnaona? Mnaona? Sasa, torati ilikuwa ni kivuli cha mambo yajayo.

⁶⁹ Hebu tufungue hapa, kwa dakika moja. Fungueni pamoja nami nyuma... Ninaamini ni mlango wa 12 wa Ufunuo. Hebu tufungue hilo kwa muda mfupi tu, tuone kama hatuwezi kupata kitu kidogo kizuri tu papa hapa, kwanza kabisa, tukiwazia juu ya “kivuli.” Sasa hebu—hebu tusome tena, sasa, wewe uliye na Biblia yako.

Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke . . .

70 *Mwanamke anawakilisha nini katika Biblia? Kanisa.*

. . . mwanamke aliyevikwa jua, (hilo lilikuwa vazi lake alilokuwa amevaa, mnaona), na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji na nyota kumi na mbili:

Naye alikuwa ana mimba, akilia, kwa utungu wa kuzaa, na kuumwa katika kuzaa.

71 Angalieni, mwanamke alionekana angani, kwa o—ono la Yohana mfunuaji. Na ninii. . . Alikuwa amevikwa jua. Na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake. Naye alikuwa na nyota kumi na mbili katika taji yake.

72 Sasa hiyo ishara ni nini? Maono ni ishara. Sasa, mwanamke ni kanisa. Nalo kanisa lilikuwa . . . Mwezi ulikuwa chini ya miguu yake. Kwa maneno mengine, ulikuwa bado unaangaza, lakini alikuwa juu yake. Kwa sababu, tayari alikuwa amefikia hali kwamba alikuwa anazaa mtoto. Alikuwa na utungu wa kuzaa. Nao mwezi ulikuwa ukipita, na jua lilikuwa linawaka. Sasa, mwezi ni . . .

73 Kinachoufanya mwezi kuangaza, ni jua kuumulika. Ni kivuli tu cha jua. Na, kwa hiyo, mwezi ulikuwa umemaliza siku yake, nalo jua lilikuwa linachomoza. Mwanamke hakuwa amevikwa mwezi. Alikuwa amevikwa jua; lilikuwa ni kanisa la Injili likichipuka. Lile kanisa la kale la Kiothodoksi. . .

Sasa, unasema, “Vema, hilo lilikuwa la Kiothodoksi?” Naam.

74 Yesu alikuja kwanza kwa Myahudi, wala sio Mmataifa. Mnaona? Yeye, Yeye aliwaagiza wanafunzi Wake wasiende kwa Mmataifa yeyote. Alisema, “Alikuja kwa walio Wake, na walio Wake hawakumpokea.” Ati nini? Alisema, wakati akiwaagiza, katika mlango wa 10 wa Mathayo Mtakatifu. Alisema, “Msiende katika njia ya Mataifa, bali nendeni kwa kondoo waliopotea wa Israeli. Na katika kuenenda kwenu, hubirini, mkisema Ufalme wa Mbinguni umekaribia.” Mnaona? “Msiende katika njia za mji wa Samaria, au njia yoyote ya hizo zingine, lakini nendeni kwanza kwa kondoo wa Israeli waliopotea.”

75 Hiyo ndiyo sababu nuru ya jua tukufu ilikuwa ikimulika kumzunguka huyo mwanamke. Naye, akiwa katika utungu, akiumwa kwa utungu, apate kumzaa Mtoto huyu.

Naye akazaa mtoto mwanamume, ambaye atayachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma: . . .

. . . na yule joka akasimama karibu na yule mwanamke aliye (Rumi) ili azaapo amle mtoto wake.

76 Na Rumi kweli ilimtesa huyo Mtoto. Walituma watu na kuwaua watoto wote, kuanzia umri wa miaka miwili

kuendelea...au, umri wa miaka miwili kwenda chini, hasa, wapate kumuua Kristo, na kumkamata mle ndani. Herode alitoa amri hii.

...lakini *mtoto* wa huyo mwanamke *akanyakuliwa* hata kwa Mungu,...

⁷⁷ Kutoka kwa ufufuo, “alinyakuliwa hata kwa Mungu, na ameketi mkono wa kuume wa Mungu.” Sasa, hiyo ingekatilia mbali mafundisho yote ya “mtoto wa kiume,” sivyo? Mnaona?

⁷⁸ Lakini sasa, “Torati,” Waebrania 10 tena, “kwa kuwa ni kivuli cha mambo yajayo,” wala si sura yenyewe, bali kivuli.

⁷⁹ Sasa, hivi majuzi usiku, nilikuwa nikijadiliana na mtu mzuri sana, juu ya fundisho la Utawala wa Miaka Elfu. Nikasema, “Ninaamini katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa sababu kuna vivuli vingi sana vya Agano la Kale vinavyosema ya kwamba kutakuwa na Utawala wa Miaka Elfu. Lazima uwepo. Vivuli vingi mno!”

Wao walisema, “Je, Kanisa litapitia kwenye ile Dhiki?”

⁸⁰ Nikasema, “La. Kanisa haliwezi kupitia kwenye ile Dhiki, halina budi kuondoka kabla ya ile Dhiki. Vivuli vingi mno!” Angalieni, kwamba, Nuhu, hapo mwanzo, Nuhu... “Agano la Kale lote, torati yote, sasa, ilikuwa ni kivuli cha mambo mema yajayo.”

⁸¹ Sasa, kabla wakati wa dhiki haujafika, kwanza, Henoko, yule...Nuhu, Nuhu alikuwa mfano wa waliobebwa wakavushwa, kama yule bikira aliyelala, lakini Henoko alihamishwa kabla tu ile dhiki haijaanza. “Henoko alitwaliwa juu, asionekane, kwa sababu Mungu alimtwaa,” mfano wa kuondoka kwa Kanisa. Ndipo Nuhu akamtazama. Alipoona Henoko akienda, alijua wakati wa kuingia katika safina ulikuwa umewadia, apate kupitishwa kwenye ile dhiki.

⁸² Biblia ilisema, “Kulikuwa na wanawali kumi waliotoka kwenda kumlaki Bwana-arusi; na watano walikuwa na busara, watano walikuwa wapumbavu. Nao wote walikuwa wanawali, kila mmoja wao. Lakini watano walikuwa na busara, nao walikuwa na Mafuta katika taa yao. Nao wakatoka kwenda kumlaki Bwana-arusi. Naye Bwana-arusi akaja, nao wale waliokuwa na Mafuta wakaingia.” Mnaona, kule kuhamishwa, kwenda pamoja na Bwana-arusi.

⁸³ Lakini wale walioachwa nyuma, walikuja na kutaka kuingia, pia. Kama tu wale waliokuja na kubisha kwenye mlango wa safina, “Nuhu, turuhusu tuingie,” lakini Mungu aliufunga huo mlango.

⁸⁴ Na, loo, rafiki yangu, moja ya siku hizi, Mungu atakupa wito wako wa mwisho. Ndipo mlango utafungwa, kati ya rehema na hukumu. Usiachwe një. Ingia sasa wakati ukiweza. Usizingatie kile ulimwengu usemacho. Ingia ndani ya Kristo. “Kwa kuwa

wale walio ndani ya Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye.” Unaona?

Basi, huyu mwanamwali mwenye busara akaondoka, katika kuhamishwa.

⁸⁵ Nao hawa wengine waliokuja na kubisha mlango, ilikuwaje? Ni nini kilifanyika? Biblia ilisema, “Walitupwa katika giza la nje, ambako kulikuwa na kulia na kuomboleza na kusaga meno.”

⁸⁶ Israeli, wakati ule wakati wa dhiki ulipoikumba Misri, hapakuwa na hata kitu kimoja kilichopata kuipiga Misri... Waisraeli, kwa sababu walikuwa katika mahali palipoandaliwa na Mungu, Gosheni. Hakuna dhiki hata kidogo. Mnaona? Wengine wote walikuwa kwenye ile dhiki, lakini sio hawa.

⁸⁷ Sasa, mambo hayo yote yakiwa ni vivuli, hayana budi kuainisha jambo fulani. Ndipo basi tunapooni kule kutangulia kuja kwa Bwana, tunaona jinsi watu walivyotembea katika siku hizo, na kuona jinsi watu walivyokuwa. “Wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu.” Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Watu wanafuata tamaa zao mbovu. Imefikia kwenye jambo... Samahani tamshi hili, dada zangu. Lakini imefikia, hata, maadili halisi ya kanuni za adabu karibu ni jambo la wakati uliopita, miongoni mwa watu wetu.

⁸⁸ Jana, katika Hospitali ya Mtakatifu Edwards, nilimsikia daktari akimkemea msichana mmoja kwelikweli huko nyuma. Alipanda vipandio ambapo ningeweza kumpa mkono, kila mtu hospitalini alikuwa akisikiliza, akitazama. Kulikuwako na msichana huko nyuma, amevaa baadhi ya nguo hizi ndogo, mbovu, kama vile maskini suruali ndefu.

⁸⁹ Mnajua yale Biblia isemayo kuhusu hilo? Anasema, “Ni chukizo mbele za Mungu, kwa mwanamke kuvaa suruali kama mwanamume.” Kweli.

⁹⁰ Naye huyo hapo, akitembe... Huyo daktari akasema... Maskini jamaa, aliyelemaa. Ninamjua, lakini siwezi kulikumbuka jina lake. Akasema, “Unataka kuniambia kuwa sista alikuruhusu uingie katika hospitali hii namna hiyo?” Kasema, “Mbona, wewe ni aibu kwa hospitali. Toka hapa.”

Nikasema, “Jamani, nataka kukupa mkono.” Hakika.

⁹¹ Kasema, “Uliwezaje kupita kule mbele? Hivi huna aibu, kuingia hapa ndani umevalia namna hiyo?”

⁹² Nikawazia, “Loo, ndugu, hiyo ni kweli.” Ninavutiwa na mtu mwenye ujasiri wa kutosha kuita mema “mema,” na mabaya “mabaya,” bila kujali yeye ni nani. Mnaona? Lakini, jambo la adabu, loo, naomba mimi... .

⁹³ Mtaniwia radhi, sivyo? Ninataka kusimama hapa kwa dakika moja tu. Sasa, nataka, huenda nikalinyoosha hili kidogo tu, rafiki yangu mpendwa. Usifikiri ya kwamba Ndugu Branham anajaribu kuwa mjuvi. Sivyo. Ninajaribu tu kusema ukweli.

Na kile nijuacho, ni kwamba huko Utukufuni, siku moja, kama ningeona maisha yako yamechafuliwa, halafu nijue ya kwamba mimi ndiye niliyesababisha hilo, na nikijua Ukweli wala nisingeusema. La, nitaliondoa mabegani mwangu, na kuliweka kwa yako. Wewe jiamulie.

⁹⁴ Wanawake wetu wanaovalia hivyo, wana pepo mchafu. Mnaona? Kuna kitu kimoja tu katika Maandiko kilichowahi kufanya hivyo. Hicho kilikuwa ni Ibilisi, aliyewavua watu nguo. Angalieni. Sasa, simaanishi kusema wewe ni mtovu wa uadilifu; simaanishi hilo, dada yangu mpendwa. Lakini uko katika mtindo wa kisasa, hivi kwamba, mpaka kwa urahisi tu wewe... Unafikiri ni vema kwa sababu wengine wanafanya hivyo, wala hutambui ya kwamba huyo ni ibilisi anayefanya hivyo. Hakika, ndiye. Wewe si maarufu. Una kichaa. Samahani tamshi hilo. Vema, hiyo ni kweli. Ninamaanisha, unaingia kichaa cha kumwacha Mungu.

⁹⁵ Loo, Roho Mtakatifu wa Mungu, hatashindana na mwanadamu sikuzote. "Hataki mtu yeyote aangamie, bali wote waifikie toba." Naye Mungu na atupe ujasiri, katika siku ambapo wahubiri... Hapa ndipo lilipoanzia, ni kwa sababu mchungaji wako, jukwaani, hulivumilia. Hiyo ni kweli. Unapaswa kutengwa. Kama ngingekuwa na kanisa, nao wanawake wafanye hivyo kanisani, mara moja wangeondolewa kwenye kitabu cha kanisa. Naam, bwana. Papo hapo, mpaka mtakapojiadibisha, muanze vizuri. Mungu awawajibishe. Lakini, siku hizi...

⁹⁶ Nilitoka nikaenda kwa Mtakatifu Yusufu. Sikuzote nawatembelea wagonjwa hospitalini, hali hizi za dharura. Nilitoka kwenda kule kuona mtoto mchanga, akifa, kansa... au ugonjwa wa figo; ametolewa figo moja, umri wa siku mbili au tatu tu. Na jinsi maskini kitoto hicho... Na hapo nikaona, katika hospitali ya Kikatoliki, wazuri sana na wakarimu.

⁹⁷ Ninaenda kwenye hospitali ya Kiprotestanti. Kulikuwa na mwanamke aliyekuwa yuafa, nami nikaenda kule kumwekea mikono yangu. Kasisi, akisimama pale, alisema... Nami nikamjulisha kwamba nilikuwa wa dhehebu moja naye. Kasema, "Huh! La! Kamwe, kamwe, kamwe! Usifanye hivyo. Usimwekee mkono wako."

Nikasema, "Biblia ilisema."

⁹⁸ "Ah, toka nje!" Kasema, "Mambo hayo si mazuri. Hapana, hatutaki umwekee mgonjwa mikono yako humu ndani." Mnaona jinsi ilivyo?

⁹⁹ Na hiyo ndiyo sababu kanisa Katoliki linawameza, kwa maelfu. Hiyo ni kweli. Kwa sababu, Protestanti haijaingia ndani ya Mungu vya kutosha kupata ujuzi, kujua wokovu halisi, wa mtindo wa kale, wa moyoni, Nguvu za Mungu, ni nini. Hilo hapo

darasa lako duni. Na hilo hapo darasa lako lililojazwa, likingojea Kuja kwa Bwana. Amina. Haya basi.

¹⁰⁰ Angalieni, “Torati ikiwa ni kivuli.” Mambo haya yote tunayoona sasa ni kivuli, yalikuwa ni vivuli, na sasa vinakuwa halisi. Ni kama tu mti unavyokua, nao unakuwa tawi; kisha unaingia kwenye mbegu, upate kutoa namna ile ile ya mbegu iliyoingia ardhini. Mambo haya yote yanatoka kwenye Mwanzo. Na, leo, sasa . . .

¹⁰¹ “Lakini waabudu hawa, waliokuja chini ya hicho kivuli, wasingeweza kufanywa wakamilifu.” Hebu tudumu kwenye neno hilo hapo.

. . . *walizitoa mwaka* baada ya *mwaka daima haziwezi kumkamilisha* akaribiaye.

¹⁰² Nawatakeni sasa . . . Hivi hamjasikia, mara nyingi, watu wakisema, “Loo, hakuna aliye mkamilifu”? Hiyo ni kweli, huwezi kuwa mkamilifu machoni pa mwanadamu mwenzako.

¹⁰³ Lakini huna budi kuwa mkamilifu, la sivyo kamwe hutaenda Mbinguni. Kweli. Biblia ilisema, Yesu akinena, katika zile heri, Mathayo; kasema, “Basi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu.” Basi, huna budi kuwa mkamilifu tu kama vile Mungu alivyo, la sivyo umepotea. Sasa utafanyaje hilo? Unaona?

¹⁰⁴ Sasa, kosa moja dogo, nawe umepotea; kufumba kumoja kudogo kwa jicho, nawe umepotea; kwa sababu hakuna kinachoweza kuingia kwenye Maeneo hayo ila “kikamilifu.” Mungu alimweka Shetani Huko juu, wakati mmoja, kama Malaika, ambaye alikuwa Mwana wa Asubuhi, naye akachukua mambo mema ya Mungu na kuyapotosha kuwa maovu. Mungu ana hakika kwamba hakuna kitakachoringia Huko kitakachoweza kufanya hivyo tena. Mnaona?

¹⁰⁵ Sasa, huna budi kuwa mkamilifu. Yesu alisema, “Iweni basi wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu.” Sasa, utakuwaje, wakati sikuzote unatenda dhambi, wakati unaendelea kufanya makosa? Sasa, hili litaweka kikwazo kidogo kwa washika sheria, lakini, angalieni. Si kile unachofanya; ni kile Mungu amefanya. Si kile unachofanya; ni kile Yeye alichofanya. Unaona? Huwezi kuwa mkamilifu; huwezi kuwa, kwa nafsi yako. Lakini, katika Kristo, umekamilishwa. Hutegemei matendo yako mema, au kanisa lako mwenyewe, bali unaitumainia Damu iliyomwagika ya Bwana Yesu. Haya basi. Hiyo ndiyo inayokufanya mkamilifu. Hiyo ndiyo inayoiimarisha imani yako.

¹⁰⁶ Halafu, juu ya uponyaji wa Kiungu, vivyo hivyo. Situmainii jinsi ninavyojisikia. Kama ningefanya hivyo, ningekuwa kitandani, asubuhi ya leo. Lakini ninaitumainia kazi Yake iliyokamilika. Yeye alisema; Yeye aliahidi hilo; ninaliamini. Mnaona? Jambo ndilo hilo. “Basi iweni wakamilifu.”

¹⁰⁷ Sasa, loo, hebu twendeni kando kidogo, kitu fulani kimebingirika moyoni mwangu. Hebu niwaulizeni jambo fulani. Tunaishi katika siku ya hukumu sasa, si ile Hukumu kuu, bali kule kuitwa kwa Kanisa litoke. Mnaamini hilo? Tunaishi katika siku za ubaguzi. Kuna u—ufidhuli, u—ubaguzi wa rangi unaojaribu kuibuka nchini. Huo ni upuuzi. Lakini kuna wakati halisi wa utengano; mema na mabaya. Mungu huwatenganisha watu Wake, huwaita watoke. Je, mnajua, neno lenyewe *kanisa* linamaanisha “waliotengwa; walioitwa watoke; waliotengwa”? Amina. “Tokeni kati yao,” Biblia inasema, “msishiriki dhambi yao na uchafu wao, nami nitawakaribisha Kwangu. Nanyi mtakuwa wana na binti Kwangu, nami nitakuwa Mungu kwenu. Tokeni!” Ni wakati wa kutengana. “Na zaidi sana mnapoona siku hii ikikaribia.”

¹⁰⁸ Kanisa ambalo wakati mmoja lilijaribu kutembea, walijiundia dhehebu, na sasa wameingia katika lundo moja kubwa la kuishi kama walimwengu. Mnaona, kama tu Biblia ilivyosema walifanya katika Agano la Kale, ndivyo walivyofanya, wengi wao. Mungu aliwaita watoke, akawaonyesha miujiza na maajabu, ndipo hicho kizazi chote kikaangamia nyikani; wakiisha kuiona miujiza, baada ya Mungu kuwafanyia miujiza, wakiisha kuuona utukufu wa Mungu. Lakini, moyoni mwao, walikuwa wasioamini, wakamnung'unikia Mungu, walalamikaji. Mungu alisema tu, “Jitenge, Musa.” Naye akaanzisha kizazi kipya, apate kuwapeleka katika nchi ya ahadi.

¹⁰⁹ Angalieni. Ni wangapi hapa ndani asubuhi ya leo walio Wakristo? Mnaweza kuinua mikono yenu, inueni tu mikono yenu, “Mimi ni Mkristo.” Mungu asifiwe, kwamba wewe ni Mkristo. Mlipataje kuwa Wakristo? Kwa sababu ulisema, “Na—nataka kuwa Mkristo”? Kwa sababu kwamba ulimtafuta Mungu, kwa machozi? Kwa sababu Mungu, kwa neema, alikuwa. Hiyo ni kweli. Si kwa sababu wewe ulimtafuta; kwa sababu Yeye alikutafuta.

¹¹⁰ Sasa, ukiangalia, kwa upande wa Wabaptisti, ama Wapresbiteri, imani ya Waarminia, wote hukauka. Wanasema, “Vema, kama Mungu aliniita, haleluya, basi niko sawa. Nitafanya nitakalo.” Hiyo inaonyesha kuwa hujalipata, wala hukuitwa. Hiyo ni kweli. Endapo Mungu alikuwa, utampenda kiungu sana, mambo ya ulimwengu yangukuwa yamekufa kwako. Hiyo ni kweli.

¹¹¹ Yule jamaa mdogo anayeketi kule nyuma akirekodi sasa. Aliniuliza, tukiingia, ambaye ni nanii wangu... mmoja wa ndugu zangu, Bw. Mercier. Naye hurekodi Jumbe mikutanoni, na mwenzi wake; Leo na—na Gene, hapa nyuma. Leo aliniambia, akiingia asubuhi ya leo, akasema, “Ndugu Branham, iliyotangulia ilikuwa ni ipi; imani huzaa upendo, au upendo huzaa imani?”

112 Nikasema, “Upendo huzaa imani. Sio imani, upendo. Huna budi kupenda, kwanza, kabla hujaweza kuwa na imani.”

113 Kwa hiyo, ukisema una imani, wala humpendi Mungu kiungu, imani yako ni bure. Unaona? Unapaswa kumpenda Mungu. Kwa hiyo, unaweza kujiunga na makanisa yote nchini, ufanye chochote ulichotaka, ufanye maungamo yote utakayo; lakini kama hakuna upendo wa kweli, halisi, wa Roho Mtakatifu, uliozaliwa mara ya pili moyoni mwako kwa ajili ya Mungu, imani yako ni bure. Haidhuru unakiri kiasi gani kwamba unamwamini Mungu, hilo halina uhusiano wowote nalo. Haina budi kuzaliwa katika moyo wa mwanadamu, ndipo una Uzima wa Milele, kamwe huwezi kutenganishwa na Mungu.

114 Sasa, kama tungekuwa na wakati, kwa kuwa si wengi wenu walio na Biblia, bali katika Kitabu cha Ufunuo. Sikilizeni sasa. Vaa kofia yako ya kuwazia, na uufungue moyo wako. Nataka kusema jambo fulani hapa sasa. Ninataka msikilize kwa makini, wakati Roho Mtakatifu akiwa karibu.

115 Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba, mpinga-Kristo angekuja katika siku ya mwisho, na ya kwamba angekuwa fidhuli sana. Na katika Mathayo Mtakatifu, pia, mlango wa 24, Yesu akizungumza, alisema, “Mpinga-Kristo atakapokuja, kwamba a—angefanana sana, kama kazi halisi ya Mungu, hata angewadanganya walio Wateule kama yamkini.” Tazama, “Kuwadanganya walio Wateule. . .”

116 Hilo “Mteule,” linatoka wapi? Kutoka kwa neno “Aliyeteuliwa.” “Angewadanganya Wateule kama yamkini.” Mnaona? Lakini haiwezekani. Mungu asifiwe kwa hilo! Haiwezekani.

117 Kama vile katika Waebrania, mlango wa 6, Yeye alisema, “Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na kuonja vipawa vya kimbinguni, na nguvu za ulimwengu ujao, kama wakigeuka na kujifanya upya hata wakatubu.” Haiwezekani. Haliwezi kufanywa. Hiyo ni kweli. Inaweza kuigwa. Inaweza kuigizwa. Watu wanaweza kutenda kana kwamba wao ni *hivi-na-hivi* na wanaweza kushawishiwa na kila jambo dogo.

118 Lakini mtu ambaye amepata kuzaliwa kwa Roho wa Mungu, mwelekeo wake—wake umelengwa kuelekea Nyota ya Kaskazini. Haleluya! Wala kuzimu yote haitamtikisa kamwe. Hiyo ni kweli. Sisemi hatafanya makosa. Sitasema hatateleza na kuanguka. Hiyo ni kweli. Lakini mara tu anapoweza kusimama kwa miguu yake tena, macho yake yanaelekeza kwenye Nyota kule, naye anaendelea mbele. Hakika. “Mteule!”

119 Sasa, Biblia ilisema, nami ninajua hilo ni Neno la Mungu aliye hai. Biblia ilisema hivi. Sikilizeni sasa. Mnaona? “Naye yule mnyama, na yule nabii wa uongo,” n-a-b-i-i, umoja. “Naye

mnyama,” mamlaka. Utatu wa kuzimu; kama tu utatu wa Mungu. Sasa angalieni.

Naye aliwafanya wote, wadogo...wakubwa, walio matajiri ama maskini, watumwa au walio huru, (wanaume au wanawake, mwanamume au mwanamke, mtoto au yeyote yule)...

...aliwafanya wote, wadogo kwa wakubwa...kutiwa chapa katika...paji la uso wao, na kutiwa muhuri kuingia katika ufalme wa giza.

¹²⁰ Sasa kuna mihuri miwili inayoendelea leo hii. Wala hamjui ni wakati gani hasa...Loo, ndugu, acha hili liingie penye kilindi sana. Hujui ni wakati gani, ambao wewe uliye mpakani leo hii, utafanya uamuzi wako wa mwisho. Hiyo ni kweli. Huwezi kuyumbayumba kwa muda mrefu sana. “Roho Yangu haitashindana na mwanadamu daima.” Kwa hivyo, unaweza kuyumbayumba kwa muda. Lakini, “Roho Yangu haitashindana na mwanadamu daima,” akiwa amekwamia mpakani.

¹²¹ Angalieni, alama ya mnyama ni alama ya ukengeufu, ibilisi, kazi za ibilisi. Yesu alisema, “Kwa ushirika wao wa kanisa”? [Kusanyiko linasema, “Hapana.”—Mh.] “Kwa theolojia yao”? [“Hapana.”] “Kwa ujuzi wao wa seminari”? [“Hapana.”] “Kwa *matunda* yao mtawatambua.”

¹²² Sasa, kwa hiyo, tunda la Roho Mtakatifu ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, fadhili, utu wema, saburi, upole. Hilo ndilo tunda la Roho. Ndipo, hilo tunda, hiyo ni alama ya Roho Mtakatifu, ikionyesha ya kwamba upendo wa Kiungu umetia nanga moyoni, na mambo ya ulimwengu yamekufa.

¹²³ Sasa, alama ya ibilisi, ni uigaji; matendo, si neema. Matendo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; unafiki, kwenda kanisani, kujifanya kuwa Mkristo; kuishi kama ulimwengu, kushughulika na ulimwengu, kutoka nje na kutenda kama ulimwengu. “Na kufanana sana,” mpaka pande zote mbili zitakuwa zikionekana sawa kabisa, “kuwapoteza walio Wateule...” Huyu hapa mfuasi wa kanisa, anayehudhuria kanisani mara kwa mara; mtu mzuri sana, huenda kanisani; mtu mzuri, mzuri kimaadili. Lakini, hata hivyo, chini kabisa katika kina cha utu wao wa ndani kabisa, hakujiwahi kuwa na ujuzi wa Yesu kukaa mle ndani.

¹²⁴ Waangalie Esau na Yakobo. Mbona, Esau alikuwa mtu mwema maradufu ya Yakobo. Hakika, alikuwa hivyo. Lakini, Yakobo alikuwa na jambo moja, “Alizingatia kwa dhati thawabu yake.” Aliona hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza, na akaihesabu kuwa jambo kuu kuliko yote duniani.

¹²⁵ Na, siku hizi, tunajaribu kuhesabu kwenda kanisani, kumsikia Dk. *Nanii* ama Ndugu *Nanii* akinena, kufanya mambo kama hayo, ama kujiunga na kanisa zuri lenye kundi zuri linaloendelea, uamsho mzuri. Tunaita huko kufanya kitu kizuri. Jambo ndilo hilo.

¹²⁶ Mungu huangalia moyo. Na, moyo wa Yakobo, haukujali lolote lijalo wala liendalo. Kulikuwa na kusudi moja thabiti kwake, hilo ni, kupata hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza.

¹²⁷ Huyu hapo mwaminio halisi, leo hii. Acha walimwengu wakuite chochote watakacho. Acha waseme wewe ni mlokole, wakitaka kusema hivyo. Walimwita Yesu, “Beelzebuli.” “Ni zaidi sana vipi watakavyowaita ninyi,” alisema. “Heri ninyi watu watakapowaudhi, na kuwanenea kila neno baya kwa uongo, kwa ajili Yangu. Furahini, na kushangilia, kwa maana thawabu yenu ni kubwa Mbinguni, kwa maana ndivyo walivyowaudhi manabii waliokuwa kabla yenu.” Mnaliona?

¹²⁸ Sasa, Muhuri wa Mungu ni nini, basi? Waefeso 4:30, ilisema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu.” Ati nini? Waefeso 4:30, ninyi mnaoyaandika. “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu.” Sasa, ninajua baadhi yao husema ni *hivi*, ama *vile*, ama *vinginevyo*. Lakini, haidhuru, Biblia ilisema, “Neno la kila mtu liwe uongo, na Langu liwe kweli.”

¹²⁹ Wengine wanasema, “Kutunza siku, ndiyo alama.” Na wengine wanasema, “Kufanya *hivi*, ndiyo alama.” Na wengine wanasema, “Kuwa shahidi wa *hili*, ndiyo alama.”

¹³⁰ Lakini, Biblia ilisema, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mliwa muhuri hata Siku ya ukombozi wenu.” Muda gani? “Mpaka Siku ya ukombozi wenu.” Inawezaje kufanywa?

¹³¹ Je, Mungu anaweza kukosea? Je, angeweza kumpa mtu Roho Mtakatifu... Na Yeye kwa kuwa hana kikomo, anajua tangu mwanzo hadi mwisho, je, angempa mtu Roho Mtakatifu, na kumwahidi Uzima wa Milele, na kisha ageuke, amwondoe kwake? Hiyo ingemfanya Yeye kuwa na kikomo, kama mimi na wewe, anayeweza kukosea.

¹³² Lakini, Mungu ashukuriwe, Baba yetu wa Mbinguni hafanyi makosa. Yeye... Hakika. Hawezi kukosea. Tangu mwanzo, Yeye hakuwa na kikomo; Naye atakuwa, mwishoni. Hawezi kufanya makosa. Yeye ni mkamilifu.

¹³³ Angalieni, sasa ninarudi kwenye—kwenye Waebrania tena. Sasa, “Basi iweni wakamilifu.” Sasa nitaruka sasa niende katika Ufunuo.

Naye aliwafanya wote, ... wakubwa, (wazee, vijana, wanaume kwa wanawake). ... watumwa na walio huru, watiwe chapa katika kipaji cha uso wao, na katika mkono wao:

¹³⁴ “Naye aliwadanganya wote isipokuwa wale ambao majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.” Aliwadanganya wote, dunia nzima, wapotofu wa kidini. Yeye alimpokea aliyejifanya Mkristo. Alimdanganya mshiriki wa kanisa. Alimkosesha mtu mwenye maadili. Alimdanganya mtu

mwema. Alimdanganya yule anayejiita mhubiri. Alimdanganya yule anayejiita Mkristo.

¹³⁵ Aliwadanganya wote kwa propaganda zake kuu, akisema, “Sisi sote ni kanisa moja kubwa, nasi sote tunapaswa kuungana pamoja, na kuwa na mambo ya ulimwengu na kanisa na serikali, pamoja. Yale . . . Tutamaliza vita vyote, milele.”

¹³⁶ Maelfu ya akina mama, mamilioni yao, watasema, “Hilo ndilo tunalotaka.” Angalia inakotoka, dada. Angalia ulipo msingi wake.

¹³⁷ “Naye akawakosesha wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo.”

¹³⁸ Sasa mko tayari? Hili hapa. Lina mitutu miwili na limejaa risasi. Lisikilizeni, sasa. “Aliwadanganya wote ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo . . .” Tangu wakati walipojiunga na kanisa? Tangu wakati wa uamsho? Majina yao yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo wakati walipoingia kanisani? Hapana. “Majina yameandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu!” Amina. Hilo latosha. Mnalipata? Hilo limechunguzwa, kwa mamia ya miaka, miongoni mwa waalimu.

¹³⁹ Lakini, angalieni, jina la Mkristo halikuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo alipokuja madhabahuni. Biblia ilisema, “Jina lake liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kote kote tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” “Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wajao, nitampa Uzima wa milele, nami nitamfufua katika siku za mwisho.” Tunaogopa nini?

¹⁴⁰ Nisikilize, ndugu yangu mchovu. Biblia ilisema, ya kwamba, “Yesu alikuwa Mwana-kondoo wa Mungu aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Angalieni. Loo, jamani! Jinsi hili linavyouchoma moyo wako! Jinsi hili linavyokupa tumaini! Huko nyuma kabisa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Shetani alipopotosha, yule mwovu; Mungu, akiwa hana kikomo, aliangalia chini kupitia mkondo wa wakati, na akaona mwisho.

¹⁴¹ Kujua tangu zamani! Ikiwa Yeye hajui mambo yote, umemwekea Mungu mipaka, umemfanya mwenye kikomo kama mimi na wewe. Lakini, Mungu hana kikomo; Nguvu za Mungu, maarifa ya Mungu, kila kitu. Yeye ni Mweza yote.

¹⁴² Huko nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wakati Shetani alipofanya ule uovu, maana Shetani niani mwake alikuwa na yale aliyotaka kufanya, naye Mungu akaona jinsi angeweza kuyazuia. Amina.

¹⁴³ Biblia ilisema, “Hapo mwanzo alikuwako Neno,” Yohana Mtakatifu 1, “naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye

Neno alikuwa Mungu,” hapo mwanzo, hapo wakati ulipoanza. Ilikuwa ni Umilele, kabla ya hapo, hapa ni katika wakati, tunaozungumzia.

¹⁴⁴ Umilele ni kama m—mfululizo wa mambo. Ha—hauishi kamwe. Ni mduara, unaoendelea milele na milele na milele. Ni gurudumu lisilo na mwisho ambalo halisimami wala halina mwisho. Lakini Shetani alikatiza mle ndani, kisha akashuka hapa chini na angeharibu kitu hicho chote.

¹⁴⁵ Lakini, Mungu aliona mahali ambapo pangekuwa na kipindi cha wakati. Naye akiwa ndiye Yule mkuu asiye na kikomo, tangu mwanzo hata mwanzo, Yeye aliangalia chini. Naye alikuwa, hapo mwanzo, Neno. Sasa, neno ni wazo lililotamkwa. Mungu akaanza kuwaza, alipoanza kuona kila mwanadamu aliyepata kuja duniani, na kila ndege, na kila kioboto, na kila nzi. Haleluya! Huyu ndiye Mungu asiye na mwisho, Mwenyezi, wa Milele, aliyeko daima. Huyu Ndiye tunayemtumikia asubuhi ya leo.

¹⁴⁶ Huko nyuma kabisa hapo mwanzo, Naye akaona ya kwamba kulikuwako na watu fulani ambao wangetaka kuokoka, watu ambao watataka kuokolewa, watu ambao watakuwa waaminifu moyoni mwao. Walitaka kuokoka. Basi, Yeye hana budi kufanya maandalizi kwa ajili ya wokovu wao, hiyo ni kweli, la sivyo hawataokoka kamwe. Naye anajua kwamba chochote kisicho kikamilifu hakiwezi kuingia Mbinguni, kwa hiyo Yeye hana budi kuwatengenezea njia ya ukamilifu. Amina. Mnaliona?

¹⁴⁷ Basi, kule nyuma, Yeye alisema, “Mimi, Mwenyewe, nitashuka ulimwenguni na kuvaa mwili wa mwanadamu, nami nitalipa ile adhabu inayohitajika hapa. Nami nitapachukua mahali hapo, na nitawafanya wakamilifu kwa maana nitawaingiza ndani Yangu, nami ni mkamilifu.”

¹⁴⁸ Ndipo Yesu aliposema, “Basi iweni wakamilifu, kama wale walivyo. . . Mungu ni mkamilifu.”

¹⁴⁹ Basi huu hapa ule mwili ulioraruliwa ambao ulipigwa na kupondwa kwa ajili ya dhambi, na kila dhambi ambayo ulimwengu umewahi kuwa nayo au utapata kuwa nayo, iliwekwa juu Yake. Na Yeye ndiye mwili ambao Yehova aliufufua siku ya mwisho pale, siku ya tatu baada ya kifo Chake.

¹⁵⁰ Na kama tuko ndani ya Mwili huo, sisi ni wakamilifu tu kama vile huo Mwili ulivyo. Amina. Haya basi. Unaingiaje ndani ya Mwili huo? Unaingiaje ndani Yake? Biblia ilisema, katika Warumi 8:1, “Sasa basi, hakuna hukumu ya adhabu kwao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mwili, bali Roho.” Hawajali kile ambacho ulimwengu unasema, au kile mtu mwingine yeyote anasema, au hata kile ambacho familia yao inasema. Wanatembea katika Roho wa Mungu, katika upendo mkamilifu, wa Kiungu. Mnaliona?

151 Unaingiaje ndani Yake? Kwa kujiunga na kanisa? Kwa kupeana mikono? Kwa ubatizo wa maji? Hapana, bwana.

152 Mlango wa 12 wa Wakorintho wa Kwanza ulisema, “Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja, na kuwa viungo vya Mwili huo.” Ndipo, basi, si yale nimefanya, kile nilicho mimi, yule niliyekuwa, wala chochote kulihusu. Ni kile ambacho Mungu amenifanyia, katika Kristo, nasi tunakamilishwa kwa Dhabihu yetu.

153 Yeye hafanyi makosa. Asingekuingiza iwapo hukustahili. Anaujua moyo wako. Hiyo ni kweli. Anajua kile ulicho. Anajua malengo yako. Anajua kile ulicho. Kuna mitego kote barabarani. Hakika, ibilisi atakufanya ujikwae. Na wewe unasema, “Sikukusudia kufanya hivyo. Mungu, unajua hivyo.” Bado wewe ni mkamilifu kwa sababu kuna Damu kamilifu inayotolewa kwa ajili yako, kila siku, na Sadaka inayotoka damu inayoning’inia mbele ya Kiti cha Enzi cha Mwenyezi Mungu. Hiyo ni kweli. Sasa, uliingiaje Mle ndani? Mungu, kwa kujua tangu zamani . . .

154 Sasa, Mungu alisema ya kwamba Yesu . . . Sasa vaeni kofia zenu. Fungua moyo wako. Tazama. Biblia ilisema, “Yesu alikuwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu” (wapi?) “msingi wa dunia.” Alichinjwa. Kwa nini? Mungu, Baba, alipotazama chini na kuona jinsi . . .

155 Yesu hakuja tu kufa kifo cha shaghalabaghala. Hakuja kamwe, kusema, “Vema, labda mtu fulani atashikwa na huruma atakapoona jinsi nilivyokufa, kila kitu.” La. La. Mungu haendeshi shughuli Yake namna hiyo. Mungu huendesha shughuli Yake kikamilifu. Hiyo ni kweli.

156 Alijua hasa kile ambacho kingetukia. Hivyo ndivyo angeweza kutabiri. Anajua hasa kile Yeye . . . “Hataki mtu yeyote aangamie.” “Hataki,” lakini, kama hana kikomo, Yeye anajua ambaye ataokoka na ambaye hataokoka. Kwa hiyo, unaweza kuwa na uhakika, ikiwa umempokea Mungu na kujazwa na Roho Mtakatifu, umetia nanga mpaka kikomo chako cha Milele. Kwa usahihi. Unaona, Yeye anatangulia kujua.

157 Sasa angalieni. Biblia ilisema kwamba, “Yesu, Mwana-Kondoo, alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Lo! Na—najua ninatenda kigeni hapa juu, lakini na—na—najisikia vizuri sana. Tazama. Ati nini? Yesu alichinjwa kabla hata ulimwengu haujapata chembe ya kwanza ya mavumbi. Yesu alikuwa tayari amechinjwa. Kwa nini? Kwa sababu Mungu . . . Hili hapa. Lishikeni. Mungu, kwa kujua tangu zamani, wakati alipokuwa Neno hapo mwanzo, alipata wazo. Sasa ni wazo tu; ndipo alipolinena, na kusema itakuwa, Yesu alichinjwa dakika ile ile Mungu aliponena Neno. Halafu? Miaka elfu nne baadaye, Yeye alikuja na kulipa hiyo gharama, ambayo Mungu alikuwa tayari amefanya huko nyuma, kwa Neno Lake. Ilibidi aje. Ibilisi

wote kuzimuni wasingeweza kumzuia asije. Mungu alikuwa tayari amelinena.

¹⁵⁸ Sasa, mwaminio, je, umevaa viatu vyako vya furaha? Sikiliza hili. Ikiwa wewe ni Mkristo, ikiwa kweli wewe ni mtoto wa Mungu, Biblia ilisema . . .

Hiyo si, "Loo, mhubiri!"

¹⁵⁹ Hiyo ni Biblia. Ilisema, "Majina yenu yaliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Loo, jamani! Wakati ule ule ambao Kristo . . . ambao Mungu alisema Kristo angeuawa, aliandika jina Lako pamoja na Lake. Haleluya! Haya basi. Jina lako liliandikwa katika . . .

¹⁶⁰ Alisema, "Naye akawadanganya wote, wakubwa, wadogo," wengi sana walikuwa washiriki wa kanisa, waliojifanya kuwa Wakristo. "Aliwadanganya wote ambao majina yao hayakuandikwa," si katika kitabu cha kanisa, lakini, "katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo" (lini?) "kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Mungu aliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, kwa Neno Lake lililonenwa. Kisha akamtuma Kristo, ile Dhabihu, kulinunua, kulikomboa kundi lilo hilo alilokuwa ameandika majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

¹⁶¹ Sasa, "Wale aliowaita, amewahesabia haki." Aliwaita kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. "Wale aliowaita, amewahesabia haki. Na wale aliowahesabia haki, amekwisha watukuza." Mungu yule yule, ambaye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, aliliita jina lako na kuliandika kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo; katika kile Kitabu, tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, tayari amekuandalia mahali Utukufuni. "Na maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibika, tunayo moja tayari inayotungoza huko Utukufuni . . . ? . . ." Haya basi. Hiyo ndiyo Injili.

¹⁶² Tunahofia nini? Kwa nini tunatembea tukionekana *hivi*, "Vema, nashangaa tu"?

¹⁶³ Inueni vichwa vyenu! Biblia ilisema, "Inueni magoti manyonge. Na mikono iinuliwe juu, ambayo wakati mmoja ilining'inia chini. Aliye dhaifu, aseme, 'Nina nguvu.'" Amina.

¹⁶⁴ Kwa maana, Injili imetolewa. Ni Habari njema. Tena, asubuhi ya leo, Roho Mtakatifu, kupitia kwa Neno, anakuletea Habari njema, kwamba, "Tangu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu Mungu aliandika jina lako katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo." Mapepo wote kutoka kuzimu hawawezi kulifutilia kutoka huko. Neno la Mungu limekwisha kulinena. Lina hakika kutukia, kama Mungu alivyoliandika mle ndani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu! Amina. Jinsi Baba

yetu wa Mbinguni alivyo na utukufu, katika upendo Wake usio na mwisho na rehema Yake, kutufanyia hayo!

¹⁶⁵ Kasema, “Basi iweni wakamilifu, kama Baba yenu wa Mbinguni alivyo mkamilifu.” Unawezaje kuwa? Wakati, sio ukamilifu wangu, sio ukamilifu wako. Ni ukamilifu Wake, wa Neno Lake; kwamba Yeye alikuchagua, wala wewe hukumchagua kamwe. Naye akakuvingiza ndani ya Kristo. Nawe umelindwa pamoja na Yesu Kristo, na mkamilifu tu kama Kristo alivyokuwa mbele za Mungu. Kwa kuwa, husimami peke yako. Unasimama ndani Yake, na jambo moja, “Ninamwamini Mungu.” Amina. Loo, ninampenda! Loo, jamani!

¹⁶⁶ Ng’ambo ya pili ya Edeni, amina, utakuwa ni wakati mzuri jinsi gani siku moja, utakapoangalia nyuma chini na kusema, “Kwa nini niliogopa? Angalieni furaha niliyokosa.”

¹⁶⁷ Kijana mwanamume, kijana mwanamke, asubuhi ya leo, ama wewe mzee ama mwanamke, ambaye hujawahi kuwa Mkristo, Mungu amebisha moyoni mwako kila mara. [Ndugu Branham aligongagonga mimbara—Mh.] Loo, naam, huenda ukaingia mwishoni mwa barabara, bali hutakuwa na furaha. Hakutakuwako na nyota karibu nawe kuangaza. Sitaki kusimama hivyo.

¹⁶⁸ Nataka kumsikia Yeye akisema, “Ilikuwa vyema, mtumishi wangu mwema na mwaminifu.” Ninataka kumwonyesha shukrani zangu.

¹⁶⁹ Maskini mke wangu, mwenye mvi, jinsi ningependa kumfanyia jambo fulani, ambalo najua analipenda, kwa sababu ninampenda, nami najua ananipenda. Na kama ningemfanyia mke wangu hivyo, katika upendo wa kibinadamu, yanipasa kufanya nini, kujua ya kwamba Mungu, kwa neema, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, aliniona; maskini, mwenye dhambi akiyumbayumba, na ameelekea kuzimu wala asingeweza kujizuia? Naye alinichagua tangu zamani, na kuweka jina langu katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Loo, ninampenda! Hakuna njia hata kidogo, ya kusema kamwe...?...Si ajabu Biblia ilisema, “Jicho halijaona, sikio halijasikia, wala halijaingia katika mioyo ya mwanadamu.” Loo, jamani! Jinsi Mungu alivyo mtukufu! Je, hutaki kumwamini, ikiwa umechoka na kutupwa huku na huku?

¹⁷⁰ Aibu kwenu Wakristo, mnaojiita Wakristo, na kwenda huku na huko mkiwa na uchovu. “Vema, sijui. Na kama nikienda kanisani, ninii...” Loo, wewe ni kisingizio duni.

¹⁷¹ Hebu nikwambie. Inueni vichwa vyenu. Nyosha kifua chako. Loo, jamani! Loo, tumieni imani. Imani ndiye bosi. Hiyo ni kweli. Imani ina nywele kifuani mwake. Ndugu, ninamaanisha, ina misuli mikubwa. Inapozungumza, wasiwasi wote huanguka kutoka upande mmoja hadi mwingine.

¹⁷² Ibilisi anasema, “Sasa, kamwe huwezi kufaulu. Huwezi kufanya hivi. Unaona aibu kushuhudia.”

¹⁷³ Imani inainuka, inasema, “Nyamaza! Nina haki ya kuzungumza.” Amina. Hakika. Imani huchukua hatua. Hiyo ndiyo tunayohitaji siku hizi kwa kila msafiri nchini. Nyosha kichwa chako.

¹⁷⁴ Biblia ilisema, “Nilipokuwa...” Daudi alisema, “Nilipohofu, nilitembea na... Nilimtumaini. Nilipohofu, basi nilimwamini. Kila ninapofikia hata hofu ya mauti, vivuli...”

¹⁷⁵ Paulo aliposhuka, alisema, “Mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako?” Ndugu...

Maisha ya watu mashuhuri yote
hutukumbusha,
Tunaweza kufanya maisha yetu adhimu,
Tunapoachana, tunaacha nyuma yetu
Kumbukumbu za kudumu.

¹⁷⁶ Siku moja, nikiwa nimeketi kule juu ya vilima vya peponi vya Utukufu, ambapo jua halitashuka kamwe katika Mji huo, ambako watakatifu tayari wanapaza sauti, wale mashujaa wa kale wa Imani, nikitazama nyuma katika sehemu hizo kule, na kuona njia yetu, iliyotengenezwa kwa Utukufu. Ninataka kuketi pamoja nao, na kuona kwamba nimeinua kichwa changu juu na kumtumaini Mungu, na kuendelea kutembea, katika wakati wa dhoruba. Loo, jamani!

Na tuombe.

¹⁷⁷ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe asubuhi ya leo kwa ajili ya Yesu. Tunakushukuru Wewe kwa ukamilifu wa Injili, kwa ajili ya kukamilishwa, na ukuu wa Milele wa Neno la Mungu la Milele, lililonenwa. Na kulingana na Neno Lake, alituita na kutuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuandika majina yetu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mungu anaposema neno, halina budi kutukia. Ni lazima tu litukie. Nawe ulinena majina yetu uliponena Jina Lake. Ulituchagua sisi, pamoja Naye, kabla ulimwengu haujaanza, kwa hiyo hakuna kitu tunachoweza kusema tunaweza kufanya, Bwana. Ha—halipo kwa wanadamu. Hakuna tunachoweza kujivunia au kujigamba juu yake. Kitu pekee tunachosema, ni, “Mungu, asante kwa neema Yako. Asante kwa rehema Zako, Bwana. Kwa kuwa tulikuwa wageni, lakini sasa Wewe umetukamilisha kwa ile Dhabihu kamilifu tunayosimama ndani yake, Ee Mungu, simama ndani Yake, leo, tunaposonga mbele.” Tukikushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya mambo haya.

¹⁷⁸ Tunaomba, kama kuna mmoja humu ndani leo, Bwana, ambaye hayuko katika hali hiyo, na wafanye uamuzi wao mmoja wa Milele na wa mwisho wakati huu, kabla hujatoa wito Wako

wa mwisho na wa kumalizia moyoni mwao. Tunaomba ya kwamba Wewe utatujalia hayo kupitia kwa Jina la Kristo.

¹⁷⁹ Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, sijui kama kuna mtu kama huyo hapa asubuhi ya leo, ambaye kweli yuko katika mwanamwali aliyelala; hujawahi kuamka na kutambua kwamba unapaswa kuwaokoa watu, inakubidi kufanya jambo fulani? Nawe unataka Mungu akukumbuke, kama mwokozi wa nafsi; unataka kuwa mmoja ambaye atatoka na kujaribu kuwaokoa watu? Naomba uinue mkono wako, useme, “Mungu, nikumbuke.” Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Vema.

¹⁸⁰ Je, kuna mtu kama huyo hapa asubuhi ya leo ambaye hajawahi kumpokea Kristo wakati mmoja kama Mwokozi, lakini, asubuhi ya leo, anataka kufanya uamuzi huo wa mwisho na wa Milele? Unapoliona jua likitua huko nje, basi ujue ni siku chache tu zaidi na hatutakuwa hapa tena. Unajua hilo. Lakini unataka—unataka kuingia katika Ufalme wa Mungu. Unataka Mungu akupokee. Nawe unaamini ya kwamba Yeye hufanya hivyo, nawe utainua mkono wako juu kwa jambo hilo, asubuhi ya leo, kwamba unaamini kwamba Kristo sasa anakuchukua kama mtoto Wake. Mungu akubariki. Na Mungu akubariki.

¹⁸¹ Mtu mwingine, utamchukua kama Mwokozi wako binafsi, leo hii? Utainua mkono wako, useme, “Kuanzia leo hii, na kuendelea, sasa nitamtumikia Mungu kwa moyo wangu wote. Naamini. Na ninataka kukumbukwa. Maishani mwangu mwote, Kitu fulani kimegongagonga moyoni mwangu, na kubisha moyoni mwangu, nami nimeukataa. Nami nahofia huenda nikaukataa wakati usiofaa sasa. Na kwa hiyo, asubuhi ya leo, Mungu, kwa neema, ninatoka na kuinua mkono wangu, nikisema, ‘Unirehemu mimi, mwenye dhambi’?”

¹⁸² Je, kunaweza kuwa na mwingine? Mungu akubariki. Na akubariki, msichana mdogo. Ninauona mkono wako, pia, mpenzi. Vema. Mtu mwingine, unaweza kuinua mkono wako, ukisema, “Nikumbuke”?

¹⁸³ Kuna aliyerudi nyuma, na aseme, “Loo, Ndugu Branham, mimi ni Mkristo, lakini mimi ni mfano duni kuwa mmoja. Sikuzote ninarudi nyuma na kufanya mabaya. Nami ni—ninampenda Mungu. Mungu alinichukua kwa neema. Najua mimi ni mtoto Wake. Lakini sijawahi kuwa mtendaji, sijawahi kufanya kazi ya Bwana. Kwa namna fulani mimi huchukuliwa tu na mkondo, na kuingia na kutoka, kuingia na kutoka. Lakini Kitu fulani kinaendelea kunishikilia, moyoni mwangu. Ninauonea aibu ushuhuda wangu. Ningona aibu kukutana na Mungu, asubuhi ya leo, bila nafsi moja ama mkono mtupu. Na—na—nataka Mungu anirejeshe na kunikumbatia kwenye ubavu Wake unaotoka damu, na kunipa kichapo changu, kile ninachostahili, na anijalie niwe Mkristo halisi tangu leo, na

kuendelea. Nitamwinulia Mungu mkono wangu. Hilo ndilo ninalotaka ufanye, Mungu.”

¹⁸⁴ Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Kwamba, sasa Mungu anauona moyo wako. Na wengi wenu mlioinua mikono yenu, ninawajua. Nayajua maisha yenu ya masumbuko. Wakati mkinii... (Wakristo wengine wanaomba.) Ninajua hali yenu ya masumbuko. Najua kurudi nyuma kwenu. Mungu anayajua vizuri zaidi, ikiwa niliyajua. Ninakuona ukija madhabahuni, ukijaribu kuanza, kisha unarudi nyuma; unajaribu kuanza, kisha unarudi nyuma.

¹⁸⁵ Mtu mmoja alianguka tu akafa, siku chache zilizopita, ambaye alikuwa akifundisha shule ya Jumapili hapa. Ninahofu baadhi ya watu wake wako hapa. Ningelitaja hilo jina, wengi wenu mnajua ninayezungumzia. Mtu huyo angekuja kanisani, angerudi nyuma; angekuja kanisani, angerudi nyuma. Alitaka kufanya mema. Alikuwa na tukio na Mungu. Alikuwa mtu mwema, moyoni, lakini alianza kujishughulisha sana na ulimwengu. Alikufa, kijana mwanamume. Aliondoka duniani. Sasa nashangaa malipo yake yatakuwaje. Mnaona? Usifanye hivyo. Usifanye hivyo, rafiki. Dumu kazini.

¹⁸⁶ Mtu huyo angeweza kurudi duniani leo, na kusimama kule mjini, popote pale, mahali pale alipofia, angepiga mayowe na kukimbia akielekea maskanini upesi alivyoweza kuja. Jamani, ninawaambia, kungekuwako na nafsi zingeokolewa juma hili lijalo, atakapofika hapa. Yuko ng'ambo ya mpaka sasa. Lakini, kumbukeni, maadamu kuna Umilele, wenye kina kirefu kama kulivyo na anga, hawatakuwa na nafasi nyingine ya kuokoa mtu, kamwe hawatakuwa na nafasi nyingine ya kumwishia Mungu. Amefanya uamuzi wake wa mwisho.

¹⁸⁷ Vipi kuhusu wako, asubuhi ya leo? Hebu tujirekebishe, kwa ajili ya Mungu, huku tumeinamisha vichwa vyetu. Tupe sauti ndogo, “Ng'ambo ya pili ya Yordani.”

Ninii ya pili . . .

Sasa endelea kuomba.

. . . ya Yordani,

Katika mashamba matamu ya Edeni,

Polepole sasa, sisi sote.

Ambako Mti wa Uzima unanawiri,

Kuna raha kwa ajili yako.

Yesu huvunja kila mnyororo,

Yesu huvunja kila mnyororo,

Yesu . . .

Ni nini kinachokuzuia?

. . . kila mnyororo,

Anapokuweka huru!

Daima, daima nitamsifu,
 Daima, daima nitamsifu,
 Daima, daima nitamsifu,
 Kwa kuwa Yeye huniweka huru!

Sasa sisi sote, pamoja, polepole.

Ng'ambo ya pili ya Yordani, (Ng'ambo tu ya
 mto kule.)

Katika mashamba matamu ya Edeni
 Ambapo Mti wa Uzima unanawiri,
 Kuna raha kwa ajili yako.

Mbona, Yesu huvunja kila . . .

¹⁸⁸ Minyororo ya kutojali, minyororo ya kidini, minyororo
 ya kimadhehebu, minyororo wa dhambi, minyororo wa
 kutokuamini.

Yesu . . . (Uwepo Wake u karibu.) . . . kila
 minyororo.

Fanya tu uamuzi wako.

Alipokuweka huru!

Daima, daima nitamsifu,

Mungu akubariki, mama.

. . . msifu,

¹⁸⁹ Mtu mwingine, acha minyororo ivunjwe kutoka pande zote.
 Hivi hutaki kuwa huru, leo? Unajifanya nini? Mbona, wewe ni
 mnyonge tu nafsiini mwako, ikiwa huko huru; Roho Mtakatifu,
 vipande vyote vimeondolewa njiani, Roho wa Mungu akishuka
 kupitia moyoni mwako. Mungu akubariki, dada.

Ng'ambo ya pili . . .

¹⁹⁰ Labda kitu kidogo cha kale kinakushikilia. Hivi hutaki
 kuokolewa? Natumaini majina yetu yamefungwa pamoja.
 Mungu akubariki, ndugu. Natumaini majina yetu yamefungwa
 pamoja, huko Utukufuni, kama nyota za Mungu, ziking'aa
 milele. Angalia na useme, "Yule pale amesimama Ndugu
 Branham."

¹⁹¹ Nitasema, "Loo, naam, ndugu. Unakumbuka kule maskanini
 asubuhi ile?"

. . . nawiri,
 Kuna raha kwa ajili yako.

Daima, daima nitamsifu, (Je, hutaki kufanya
 hivyo?)

. . . daima, daima nitamsifu,
 Ni . . .

¹⁹² Wewe uliyerudi nyuma, hutaki kuja madhabahuni sasa?

. . . kila . . .

Kitu hicho kidogo cha kale kinachosimama njiani mwako.
Yesu huvunja mnyororo huo. Njoo.

Anapokuweka huru!

Pale msalabani alipofia Mwokozi wangu,
Huko chini kwa ajili ya kutakaswa na dhambi
nililia;

Loo, hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;
Utukufu kwa Jina Lake!

Loo, utukufu kwa Jina Lake la thamani!

Loo, utukufu . . .

¹⁹³ Rafiki mwenye dhambi, hapa madhabahuni, uliyerudi
nyuma, mwambie habari zake sasa. Ilikuwa wapi?

Huko moyoni mwangu . . .

¹⁹⁴ Unapiga magoti hapo peke yako pamoja na Mungu sasa.
Anakutazama. Hata shomoro asingeweza kuanguka bila Yeye
kujua.

Loo, njoo kwenye Chemchemi hii tajiri, tamu,
tulivu,

¹⁹⁵ Kama hujawahi kumpokea Roho Mtakatifu, njoo. Yuko
hapa.

. . . miguuni pa Mwokozi;
Loo, jitumbukize leo hii, na ufanywe mzima;
Loo, utukufu kwa ninii Lake . . . (Shikilia hapo
sasa.)

¹⁹⁶ Huku mmeinamisha vichwa vyenu. Je, umewahi kuona watu
wanaompokea Kristo? Angalia walikuwa mahali pa namna
gani, jinsi walivyompokea, unawaona wakitenda vivyo hivyo.
Hakika. Ikiwa ni ya uzushi, na kusisimkwa na mihemko, mtoto
atalelewa hivyo. Hivyo ndivyo itakavyoenenda. Ikiwa ni baridi,
la kawaida, na lisilojali; kwa kawaida ndivyo wao walivyo.
Wanapokea roho ya aina hiyo, kwa sababu hiyo ndiyo inafanya
kazi hapo wakati huo.

¹⁹⁷ Nipeleke msalabani. Nipeleke mahali ambapo pana Roho
inayotenda kazi, ambayo inautuliza moyo wangu. “Nijaposema
kwa lugha za wanadamu na Malaika, nijapotoa mali yangu yote
kuwalisha maskini, mwili wangu kuteketezwa kama dhabihu,
nina ujuzi wa kujua siri zote na mambo haya yote, yote
yatashindwa. Lakini kile kilicho kamili kitakapokuja, ambacho
ni upendo, unadumu milele.” Upendo huleta imani.

¹⁹⁸ Si uje sasa huku hisia hii ya kupendeza, nyenyekevu, tamu ya
Roho Mtakatifu ikitembea hapa madhabahuni sasa. Piga magoti
tu, useme, “Mungu, unirehemu. Nataka unipe sasa, moyoni
mwangu, Roho huyu aliye kanisani. Sasa ninapiga magoti, na
ninaomba. Na, kwa imani, ninaamini ya kwamba utanijalia.”

Utaondoka hapa, moja ya roho nyenyekevu zaidi, tamu zaidi.
Yote yatakwisha basi.

Nimeokolewa kutoka dhambini kiajabu sana,
Yesu anakaa ndani kwa utamu sana,
Loo, pale msalabani ambapo aliniingiza;
Utukufu kwa Jina Lake!

Utukufu . . .

¹⁹⁹ Wakati tukiimba huu, nashangaa kama kuna Wakristo wowote wangependa kuweka maisha yao wakfu upya pamoja na hawa hapa madhabahuni, ambao wamekuja kwa ajili ya Roho Mtakatifu na wokovu. Je, ungependa kupiga magoti pamoja nasi hapa, kuomba pamoja nasi kwa dakika chache? Chochote unachohitaji, haijalishi ni nini. Ikiwa ni ugonjwa, unahitaji kuponywa. Ikiwa ni shida, na unahitaji usaidizi, ikiwa una hofu na wasiwasi, unahitaji—unahitaji amani, njoo sasa, sivyo?

Loo, njoo kwenye Chemchemi hii tajiri na tamu;

Itupe maskini nafsi yako kwa Mwokozi . . .

Nina furaha sana kuona wengi wanakuja, asubuhi ya leo.

. . . ndani leo na kufanywa mkamilifu;

Utukufu kwa . . .

²⁰⁰ Unaona, ni kazi ya Roho Mtakatifu. Anafanya hivi. “Kwa . . .” Sio mhemko. Imara, yenye kilindi. Sio kishupavu. Sio baridi. Ni upendo unaotuvuta, unaotubidiisha.

Hapo Damu ilipakwa moyoni mwangu;

Loo, utukufu kwa Jina Lake!

²⁰¹ Ajabu! Kila mtu anainama tu sasa. Je, hamuupendi huu? Sijui mnavyojisikia, lakini ninahisi tu, moyoni mwangu, unahisi tu matone ya machozi ndani yako, yakishuka. Roho Mtakatifu wa Mungu akitembea tu, Yeye anafanya kazi hiyo. Ndugu, nipe kanisa kama hilo, ambalo kweli limevunjika, likishuka kwenda kwenye nyumba ya Mfinyanzi, kufinyangwa upya.

Yesu, unihifadhi karibu na msalaba,

Kuna Chemchemi ya thamani,

Bure kwa wote . . .

²⁰² Hebu wasikilizaji wasaidie kuimba huo sasa, huku waliotubu wakiwa madhabahuni, wakiomba.

Inatiririka kutoka kwenye Chemchemi ya Kalvari.

Msalabani, msalabani,

Loo, uwe utukufu wangu daima;

Ndipo nafsi yangu iliyonyakuliwa itapata

Raha ng'ambo ya mto.

²⁰³ Ee Mungu, Baba yetu, tunakuja Kwako, leo, kwa unyenyekevu, tumevunjika. Roho Mtakatifu akija katika

Neno. Wakristo wanashuku...na wanakushukuru Wewe sana, kwamba wamekukubali, wamezaliwa mara ya pili. Wewe umeagiza haya tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Umeyatangaza. Ulisema, "Nina mambo mengi ya kuwaambia, ambayo siwezi kuwaambia sasa. Lakini Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja, atawafunulia mambo haya, na atawafundisha na kuwaongoza." Tunashukuru sana, asubuhi ya leo, kwa ajili ya Roho Mtakatifu anayelifunua Neno la Mungu. Ulisema, "Naye ataleta vitu hivi kwenye ninii Yangu...atawakumbusha, yale niliyowaambia. Na mambo yajayo atawapasha habari zake."

²⁰⁴ Tuna furaha sana kwamba Yeye yuko pamoja nasi leo. Na kwa njia ya mafundisho ya Neno, na utendaji kazi wa Roho Mtakatifu, amewafanya Wakristo waamke, akawafanya wenye dhambi waje Kwako, waliorudi nyuma wajiweke wakfu tena. Baba, wako madhabahuni. Aliwafanya wagonjwa na waliochoka, walioteseka, waje na kuinamisha vichwa vyao, wakubali uponyaji kwa ajili ya miili yao, tukijua ya kwamba Neno Lako lililonenwa ni la Kweli. Kila kitu kingine kitashindwa, bali Neno Lako haliwezi kushindwa kamwe. Ukweli! "Mtaifahamu Kweli, nayo hiyo Kweli itawaweka huru."

²⁰⁵ Nasi tunakuja kukubali, asubuhi ya leo, kile ulichotuandalia Wewe, katika mateso Yako kwa ajili yetu na upatanisho, wakati wa kifo Chako, ulichotufanyia sisi. Nasi, Bwana Yesu, tunapokea bure. Tunaamini Neno la Mungu. Tunaamini kwamba Wewe uliahidi, "Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe." Ee Mungu, ni ahadi iliyoje! Haijalishi ni ya nini, Wewe umesema, "Mnapoomba mkisali, aminini kwamba mnayapokea mliyoomba. Yatakuwa yenu."

²⁰⁶ Sasa, Baba, kama kweli tukiliamini, limetimizwa. Tunaliamini. Limetendeka. Ndipo tunatenda kulingana na maungamo yetu, ya kwamba Wewe umetufanyia. Si kwamba tunastahili; hatustahili. Lakini kwa neema Yako isiyostahiliwa tuliyo nayo kupitia Kwako, tunaamini ya kwamba hiyo kazi imekamilika.

²⁰⁷ Na wakati hawa waliotubu, na wale wanaokuja asubuhi ya leo, wakijiweka wakfu, na kwa wale wanaokuja kwa ajili ya faida za mateso, kama Daudi alivyosema, "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana, wala usizisahau fadhili Zake zote; Yeye anisameheaye maovu yangu yote, maasi yangu; na anayeponya magonjwa yetu yote." Hizo ndizo faida za mwaminio. Nasi tunaipokea, kwa imani, asubuhi ya leo, kwa kulijilia Neno la Mungu, lililonenwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Kama isingewezekana isitendeke, basi haiwezekani sisi tusipate kile tunachoomba, tukiomba kwa imani tukiamini. Na hilo liko ndani ya mioyo yetu, Bwana, kupokea kile tulichoomba.

²⁰⁸ Yesu, utuweke karibu na msalaba. Adui ajapo kama mafuriko, Bwana, inua kiwango dhidi yake. Libariki kusanyiko

hili dogo, linalongojea. Mungu, Roho Wako Mtakatifu awachukue hawa walioweka maisha yao wakfu, wanaume na wanawake hawa waliopiga magoti madhabahuni. Wale wenye dhambi wanaokuja na kuinamisha vichwa vyao, wapeleke kwenye Ufalme Wako.

²⁰⁹ Bwana, ninatambua kwamba ni hali yao wenyewe ya kibinafsi, dakika ile waliyokuamini, hiyo ndiyo dakika uliyowapokea. Kwa maana ulisema, “Hakuna mtu angeweza kuja asipovutwa na Baba Yangu. Na wote wajao, nitampa Uzima wa milele, nami nitamfufua kwenye siku ya mwisho.” Hilo ni Neno Lako, Bwana. Tunaamini Hilo.

²¹⁰ Na imekamilika, kazi imekwisha, na tunakushukuru Wewe kwa ajili yake. Tunakushukuru kwa uponyaji wa kila mwili, kwa kila nafsi iliyochoka, kwa kila jambo ambalo nanii Wako... Wale ambao walikuwa na mikono dhaifu inayoning'inia chini, wale ambao wamekuwa waoga, wale ambao wameshangaa. Daudi alisema, “Nilipogopa, nikahofu, ndipo nilikutumaini Wewe na kuendelea.”

²¹¹ Mungu, jalia tuinue vichwa vyetu, asubuhi ya leo; sio waoga, bali Wakristo wanaomwamini Yesu Kristo. Na tuendele, huku ushuhuda wetu uking'aa. Jalia, kupitia uponyaji wa miili yetu, kupitia ushuhuda wa wokovu wetu, jalia tuwavute wengine Kwako. Tujalie, Baba, wakati yote kwenye madhabahu tunayaweka. Jalia kwa ajili ya Utukufu Wako, tunapokuamini Wewe na kukungojea Wewe, Bwana.

²¹² Hapa ndipo, kuogelea tu katika uzuri Wako, kuogelea tu katika ahadi Yako, nikimhisi huyo Roho Mtakatifu mtukufu akituvuta Kwako. Jinsi tunavyokupenda! Jinsi tunavyokusifu!

²¹³ Jinsi ninavyokuabudu, Bwana! Mimi mwenyewe, hapa nyuma ya dawati hili takatifu, huku nimekwinulia Wewe mikono yangu, ninakuabudu, Mungu wangu. Ninakuabudu. Wewe ni Mponyaji wangu, Mwokozi wangu, Mfalme wangu, Mpaji wangu, Baba yangu, Ndugu yangu! Yote kwa yote kwangu hupatikana Kwako. Wewe ndiwe nguvu zangu. Mimi hadharani... Wewe... Daudi alisema, “Nitakusifu katika kusanyiko la watakatifu.” Nami nitakupa sifa mbele ya hao waliotakaswa asubuhi ya leo. Ninakusifu kwa kuniponya. Ninakusifu kwa ajili ya maisha yangu. Ninakusifu kwa ajili ya afya yangu. Ninakusifu kwa wema ulionionyesha Wewe. Ninakusifu kwa ajili ya marafiki zangu. Ninakusifu kwa kila jambo, Bwana. Wewe ni wa ajabu, furaha isiyoelezeka na umejaa utukufu! Jinsi ninavyokusifu Wewe!

²¹⁴ Jinsi ninavyoweza kukupendekeza Wewe kwa waliochoka! Jinsi ninavyoweza kutangaza uzuri Wako kwa mwenye dhambi, kama Mwokozi! Jinsi ninavyoweza kukupendekeza Wewe kwa wagonjwa, kama Mponyaji! Jinsi ninavyoweza kutangaza uzuri Wako kwa mzururaji, kama Mfalme! Loo,

jinsi ninavyokupenda Wewe, asubuhi ya leo! Jinsi ninavyoweza kukutangaza—kukutangaza uzuri Wako, Bwana, kwa wale wanaonyanyaswa, kuwa—kuwa shangwe za furaha kambini! Jinsi tunavyokushukuru Wewe!

²¹⁵ Ee, Wewe ni Mwamba katika nchi ya uchovu, Kimbilio katika wakati wa tufani; Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Ua la Uwandani, Ninyoro ya Mabondeni, Nyota ya Asubuhi! Loo, jinsi tunavyokupenda Wewe! Jinsi tunavyokuabudu na kukusifu, Wewe wa Milele usiye na kifani! Tunakupa Wewe sifa. Loo, tutakusifu, na kukupa sifa, kupitia nyakati zote!

²¹⁶ Utupokee, Bwana, tunapotoa baraka hizi, matunda ya midomo yetu. Ulisema, “Sisi ni watu wa kipekee, ukuhani wa kifalme, tukitoa dhabihu ya kiroho, matunda ya midomo yetu tukitoa sifa kwa Jina Lake.” Jinsi tunavyomsifu! Jinsi tunavyomwabudu milele na milele! Ee, pokea sifa za mioyo yetu, elezea midomo yetu, Bwana, kwamba kutoka kwa kina cha moyo safi tunakusifu Wewe. Tukijua, kwamba, si kile tungeweza kufanya. Sio maisha yetu; ni Maisha Yake. Sio wokovu wetu; ni wokovu Wake. Sio mbingu yetu; ni Mbingu Yake. Loo, sisi si kazi zetu wenyewe; sisi ni kazi Zake. Sio neema yetu; ni neema Yake. Si utukufu wetu; bali utukufu Wake. Si nguvu zetu; bali nguvu Zake. Loo, jinsi tunavyokupenda Wewe! Si kanisa letu; bali Kanisa Lake. Jinsi tunavyokusifu Wewe, kwa kuwa hiyo ndiyo mioyo yetu, Bwana. Hiyo ndiyo mioyo yetu. Tupokee.

²¹⁷ Ee Mungu, tumia Maskani ndogo ya Branham kumwagwa kwa Roho. Sivyo, Bwana? Loo, sisi ni wahitaji, hapa pembeni. Mungu, teremsha mvua za baraka. Mimina mvua ya Mungu, ya masika na ya vuli.

²¹⁸ Mbatize mchungaji wetu, upya, Bwana. Mtie moto kwa Injili. Tunampenda, leo, Bwana. Yeye ni mtumishi Wako. Tunaomba ya kwamba utaupaka moyo wake.

²¹⁹ Paka mafuta mioyo ya wahubiri wengine humu jengoni asubuhi ya leo, na kila mshiriki. Jalia tutoke hapa, Bwana. . .

²²⁰ Na usimsahau maskini mtumishi Wako, asiyestahili, mimi, Bwana. Kwamba utanitia mafuta upya kwa Roho Mtakatifu. Tujalie, Bwana.

²²¹ Tupe baraka hizi. Tunangoja madhabahuni kwa unyenyekevu, tukijua ya kuwa tunaipokea, tukiogelea katika Roho Wako Mtakatifu; na bila kuionea haya Injili ya Yesu Kristo, Nguvu za Mungu, ziletazo wokovu. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili Yake!

²²² Siku moja tukufu, tunatumaini kukuona Wewe, Bwana, tukiweka mikono yetu juu ya miguu ya Yule anayesimama pamoja nasi leo, ambaye hatuwezi kumwona, lakini tunajua ya kwamba Yeye yuko hapa. Jinsi tunavyomsifu!

...chini katika Mji huo,
Jua halitazama kamwe;
Maua yanachanua milele,
Na jua halitatua kamwe.

Ninajisikia kuendelea na safari, najisikia,
Ninajisikia kuendelea na safari;
Maua yanachanua milele,
Na jua halitatua kamwe.

Ni wangapi wanajisikia hivyo? Inua mkono wako.

...jisikia kupaza sauti, wakati mwingine
najisikia,
Najisikia kupaza sauti, najisikia;
Maua yanachanua milele,
Na jua, halitatua kamwe.

Najisikia kuendelea na safari, najisikia,
Najisikia kuendelea na safari;
Maua yanachanua... (...?...)

²²³ Wewe Ndiwe uliye kichwani mwa mashua, Bwana. Unajua yote kuihusu. Tunaomba baraka hii katika Jina la Kristo. Amina.

²²⁴ Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunaposhuka madhabahuni, tukiweka mikono juu ya wale ambao labda wanangojea baraka zaidi, naomba Roho Mtakatifu, ambaye hakugusa tu katika njia ifaayo... Lakini tunaomba, Baba wa Mbinguni, kwamba utatujalia baraka...?... Loo, nena, Baba wa Mbinguni, umrehemu dada yetu.

²²⁵ Mpendwa Baba wa Mbinguni, mwanamke huyu mpendwa hapa anapopanda hapa kwa imani... Siku nyingi amekuwa hapa; hizi mvi na makunyanzi...?... Lakini jinsi kazi ngumu sana ingehitajika kupitia hapa. Hapana shaka mikono hii imeshuka kwenye kurasa za Biblia, ikiinuliwa Kwako. Hapana shaka, lakini ni mwaminifu moyoni, asubuhi ya leo, alipochopea akaingia humu kanisani, akiwa na mkongojo chini ya mkono wake. Lakini sasa, kwa imani, anauweka chini, ili aondoke. Mponye, Bwana. Anakuja kwa ajili ya baraka za Mungu. Ninaomba, Mungu wa Mbinguni, ya kwamba utambariki. Na jalia asilazimike kuuchukua tena, siku zake zote. Mpe nguvu katika mwili wake. Jalia awavute watu Kwako, Bwana, kwa Ufalme wa Mungu. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

²²⁶ Mungu akubariki, dada. Usininii... Hutalazimika kutumia mkongojo huo wa kale, siamini, tena. Uko mzima, nami ninaamini unaenda nyumbani bila huo. Amina. Unapotoka nje ya jengo, uweke begani mwako, kisha utoke nje. Yote yatakwishia.

²²⁷ Baba Mungu, tunaomba ya kwamba utambariki mwanamke huyu aliyesimama hapa leo. Mpe afya kabisa. Tujalie, Baba.

Tunaweka mikono juu yake na kuamini jambo hilo, katika Jina la Yesu.

²²⁸ Baba Mungu, tunaweka mikono juu ya Dada Slaughter, na tunaomba aponywe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²²⁹ Mungu mpendwa, tunaweka mikono yetu juu ya nanii wetu. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²³⁰ Hujui jinsi unavyohisi. Nitaimba ubeti huo; ninyi muimbe pambio pamoja nami.

Wa kwanza kufa kwa ajili ya mpango huu wa
Roho Mtakatifu,
Alikuwa ni Yohana Mbatizaji, alikufa kama
mwanadamu;
Ndipo akaja Bwana Yesu, wakamsulubisha,
Yeye alihubiri ya kwamba Roho angewaokoa
watu kutoka dhambini.

Inaendelea kudondoka damu, naam,
inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, (Ninaipenda.)
inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi (Acha ulimwengu useme
watakacho.) ambaye alikufa kwa ajili ya
Ukweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu inaendelea
kudondoka damu.

Kisha wakampiga mawe Stefano, alihubiri
dhidi ya dhambi
Akawafanya wakasirike sana, wakakiponda
kichwa chake;
Lakini alikufa katika Roho, akakata roho,
Ndipo akaenda kujiunga na wengine, lile jeshi
litoalo uhai.

Iliendelea kudondoka damu, . . .
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
Kweli,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu.

Kulikuweko na Petro na Paulo, na Yohana
mtakatifu,
Waliyatoa maisha yao kusudi Injili hii ipate
kuangaza;
Walichanganya damu yao, pamoja na manabii
wa kale,
Kusudi Neno la kweli la Mungu lipate
kuhubiriwa kwa uaminifu.

Inaendelea kudondoka damu, naam,
 inadondoka damu,
 Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
 Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
 Kweli,
 Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu.
 Nafsi chini ya madhabahu, wakilia, "Hata
 lini?"
 Bwana kuwaadhibu wale waliofanya mabaya;
 (Sikilizeni.)
 Lakini kutakuwa na wengine ambao watatoa
 damu ya maisha yao,
 Kwa ajili ya Injili hii ya Roho Mtakatifu na
 mafuriko Yake mekundu sana.
 Loo, inaendelea kudondoka damu, naam,
 inadondoka damu,
 Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu,
 Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
 Kweli,
 Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka . . .

²³¹ Ni wangapi walio na furaha asubuhi ya leo kwamba
 umempokea Roho Mtakatifu? Inueni mikono yenu. Je, si ni
 ajabu? Hakika.

Inadondoka . . .

²³² Peana mikono na rafiki yako anayesimama karibu nawe.

. . .dondoka damu,

Sema, "Bwana asifiwe, ndugu, kwa wema Wake wote."

. . .Injili ya Roho inadondoka damu,

Loo, damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili
 ya Kweli,

Hii . . .

Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki.

. . .Injili inadondoka damu.

Loo, inadondoka damu . . .

Jambo ndilo hilo. Inueni mikono yenu.

. . .inadondoka damu,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu,
 Damu ya wanafunzi waliokufa kwa ajili ya
 Kweli,

Injili hii ya Roho Mtakatifu inadondoka damu.

Inadondoka damu, (Haleluya!) inadondoka
 damu,

Injili hii ya Roho Mtakatifu, loo, inadondoka
 damu, (. . .? . . .)

...damu, naam, inadondoka damu,
Injili hii ya Roho Mtakatifu, inadondoka damu.

Kila mtu auimbe!

Damu ya wanafunzi...

²³³ Mungu akubariki, dada. [Dada huyo anasema, “Ndugu Branham...?...—Mh.] Naam. [“...?...miaka mitatu iliyopita.”] Ajabu! Nimefurahi sana kusikia hivyo. [“Aliniambia, ikiwa ningepata nafasi ya kuzungumza na wewe, nikwambie, ‘Aloo.’”] Mungu akubariki!

²³⁴ Mama mmoja aliyeombewa hivi punde; amekuwa akitembea sasa kwa miaka mitatu, akimtukuza Mungu.

Sasa hebu tuimbe wimbo huu mzuri wa kale. Wangapi wanaupenda huu?

Imani katika Baba, imani katika Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, watatu katika
Mmoja;

Vema, dada, tupe huo.

Imani katika...Mwana,
Imani katika Roho Mtakatifu, watatu katika
Mmoja;

Pepo watatetemeka, na wenye dhambi
wataamka:

Loo, imani katika Yehova itaninii chochote...

²³⁵ Ni wangapi wanapenda umati mzuri wenye furaha kama huu? Mbona, Mungu akubariki, dada. Hebu tuimbe sote sasa. Kila mtu, kwa sauti yao yote. Mungu akubariki, dada. Asante, dada. Mungu akubariki. Amina. Mungu akubariki. [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Ndiyo. Amina. Amina. Mungu akubariki. Mungu akubariki.

²³⁶ [Dada mmoja anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu akubariki, dada yangu mpendwa. Mungu akubariki, dada.

²³⁷ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...mikono yako, na uimbe sasa.

Mungu awe nanyi hata tutakapokutana...

²³⁸ Mungu akubariki, Dada Kelly. Nina furaha sana kukuona hapa! [Dada Kelly anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Kweli. Mungu akubariki.

²³⁹ Kila mtu anajua huyu ni nani anayepaza sauti. Ni Dada Kelly. Mnajua, alipaswa...I—ibilisi alijaribu kumwua huku nje, kwenye ajali ya motokaa, ndipo wakamlaza kule hospitalini, amekawatwa kabisa, ndipo wakasema hatatembea kamwe, na kila kitu. Lakini, neema ya Mungu! Yeye ndiye aliyeponywa. Inasikika kama Jeshi la Wokovu hapa asubuhi ya leo. Hebu

tumsifu Bwana pamoja naye, kila mtu! Njoni nyote, mkutane na Dada Kelly, na kupeana mikono naye mnapopitia.

²⁴⁰ Najua nyote mmefurahi kumwona dada yenu. Na, hapa, shukeni mkamsalimie kwa mikono, papa hapa madhabahuni. Nyote njoni, kila mtu. “Nimefurahi kukuona!” Vema, Bwana asifiwe!

Hata twonane! hata twonane!

Mungu awe nanyi hata twonane tena!

Ndugu Neville.

Hata twonane! hata twonane!

Hata twonane miguuni pa Yesu; (Hata twonane!)

Hata twonane! hata twonane!

Mungu akubariki, Ndugu Neville. Amina. Mungu akubariki.

²⁴¹ Hebu tusimame na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, sivyo, wakati ndugu akituruhusu kuondoka. Inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja katika maombi. Ndugu Neville, tafadhali.



KITABU CHA UZIMA CHA MWANA-KONDOO SWA56-0603

(The Lamb's Book Of Life)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 3 Juni, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org